Jumamosi Aprili 27, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0579903

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




UKURASA 13



## Ripoti yawaweka mtegoni wakurugenzi halmashauri

UKURASA 3

# Magufuli aingilia kati usajili laini kwa vidole



• **Asema** mamilioni watakosa mawasiliano, akiagiza uchunguzi mtoto wa miaka minne anayedaiwa kulawitiwa na baba wa miaka 53... *Endelea ukurasa 2*



Sehemu ya wananchi wa Jiji la Mbeya, waliohudhuria mkutano wa hadhara wa Rais John Magufuli, katika viwanja vya Ruanda, Nzovwe, jana. **Picha ndogo:** Rais Magufuli akiwapungia wananchi hao baada ya kuwasili. **PICHA: IKULU**

## Kimbunga Keneth chabadili mwelekeo

UKURASA 3



## Sugu aomba kazi kwa Rais Magufuli

UK.2

**MICHEZO** SIMBA YAMPELEKA TUYISENGE YANGA UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# JPM aingilia kati usajili laini za simu kwa vidole

**Na Waandishi Wetu**

RAIS John Magufuli ameingilia kati suala la usajili mpya wa laini kwa kutumia alama za vidole akiagiza uende sambamba na utoaji wa vitambulisho vya taifa.

Amebainisha kuwa hadi sasa, wananchi wenye vitambulisho vya taifa ni milioni 14 tu kati ya 55 wanaokadiriwa kuwapo nchini, hivyo kuna hatari mamilioni ya wananchi wakaachwa bila mawasiliano ya simu pale laini za simu zisizosajiliwa kwa utaratibu mpya zitakapozimwa.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo jana mjini Mbeya katika mkutano wa hadhara uliofanyika Viwanja vya Ruanda Nzovwe wakati akizungumza na wananchi ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya siku nane mkoani humo.

Alisema amesikia kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA) imetoa mwisho wa usajili wa mpya laini za simu kuwa ni Desemba mwaka huu huku ikitaka wananchi wasajili laini zao kwa kutumia vitambulisho vya taifa.

"Hesabu za kawaida Watanzania tupo milioni 55 na hadi sasa vitambulisho vya taifa vilivyotolewa ni milioni 13 au 14, sasa ukizungumza watu wote wasajiliwe wakati Nida (Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa) haijakamilisha utolewaji wa vitambulisho kwa watu wote, maana yake watu milioni 20 sasa wasiwe na simu," alisema.

Rais Magufuli alisema hawawezi wakaenda kwa utaratibu huo kama vitambulisho vya taifa havijatolewa kwa watu wote.

"Hiki ni kitu ambacho hakiwezekani, kwa hiyo TCRA na Wizara ya Mawasiliano, najua suala ambalo wanalifanya ni zuri la kusajili, najua kila nchi duniani zinafanya hivyo kupunguza ujambazi na ugaidi, lakini waanze kwa wale wenye vitambulisho waliopo ambao ni milioni 14 na wengine wapewe muda hadi mwezi Desemba," alisema.

Mbali na suala hilo, Rais Magufuli pia alitangaza kubadilisha matumizi ya eneo lililotengwa kwa ajili ya uwanja wa ndege Songwe na kuwapa wamachinga ili walitumie kufanya biashara zao.

"Sina ujanja, mnataka nitamke

INAENDELEA UK. 8



Wakazi wa jiji wakipata kifungua kinywa cha kahawa, katika eneo la Msimbazi, jijini Dar es Salaam jana. PICHA: MIRAJI MSALA

# Sugu amwomba kazi Rais Magufuli

**Na Romana Mallya**

MBUNGE wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi, maarufu Sugu (Chadema), amemwomba Rais John Magufuli kuwa msuluhishi wa kile alichokiita 'mafundofundo' ya kisiasa ndani ya Mkoa wa Mbeya na hata kitaifa, ikibidi.

Sugu alitoa ombi hilo mbele ya Rais Magufuli mjini Mbeya katika mkutano wa hadhara uliofanyika Viwanja vya Ruanda Nzovwe, alipopewa nafasi ya kuzungumza na wananchi ikiwa ni sehemu ya ziara ya siku nane ya Rais mkoani humo.

Katika hotuba yake fupi iliyoonekana kumfurahisha Rais Mgufuli, Sugu alisema: "Mimi ni kijana wako, najitolea ikikupendeza niwe 'channel ya dialogue' kuondoa mafundofundo ya kisiasa katika ngazi ya Mkoa wa Mbeya hata kitaifa ikiwezekana..."

Sugu alikatishwa kuzungumza na mshereheshaji wa mkutano huo, lakini Rais Magufuli aliagiza apewe muda zaidi wa kumalizia hotuba yake.

"Kuna watu wa Chadema wapo nyuma na wewe umesema hutaki vyama, nimekuja nimekushika ninakufuata, mimi nakuunga mkono bila kuhama chama, nitakuunga mkono hadi mwisho kwa kuwa mimi ni kijana wako," Sugu alimwahidi Rais Magufuli.

Alimweleza Rais Magufuli kuwa amepata taarifa Mwenyekiti wa Chadema Mkoa wa Mbeya amekamatwa kwa madai kuwa alikuwa akipanga kufanya fujo katika ziara yake hiyo mkoani Mbeya.

Alisema haiwezekani watu na akili zao wakae wapange wafanye fujo dhidi ya kiongozi huyo mkubwa nchini.

Alisema mwaka jana, kipindi kama hicho, akiwa gerezani, alisikia kwenye redio kuwa Rais Magufuli anakwenda Iringa na alitamani kukutana naye kwa ajili ya mazungumzo.

"Nikasikia umeondoka, nikasema inshallah, utakuja tena na kutanikuta uraiani, leo umekuja," Sugu alisema.

Kuhusu changamoto zinazokabili mkoa huo, Sugu alimweleza Rais Magufuli kuwa tatizo la maji linaweza kutatuliwa ikiwa Sh. bilioni 70 zitapatikana ili kuyatoa kwenye chanzo cha Mto Kiwira na yatahudumia pia Mkoa wa Songwe.

Akizungumzia matatizo ya wamachinga, mbunge huyo alisema matatizo yao hayawezi kutatuliwa kwa kutengwa maeneo kwa ajili yao kwa sababu hata nchi nyingine wako kila sehemu lakini wanafuata taratibu.

Alisema mfano mzuri ni jengo la Machinga Complex lililoko Dar es Salaam ambalo nalo limekuwa na changamoto kwa wamachinga.

"Suala la Machinga nakuunga mkono kwa asilimia 100, vipo vitu vingi tunakuunga mkono, lakini hawataki kukwambia kama tunakuunga mkono, lakini hata kama hawakuambii, haiondoi uhalali mdogo wa kutoa mawazo yetu na yote huwa ya unyenyekevu," Sugu alisema.

Baada ya kuwasilisha hotuba yake hiyo, Sugu alikwenda kumpa mkono Rais Magufuli ambaye alionekana kukoshwa na maneno yake kiasi cha kumpigia makofi.

## Rais asamehe wafungwa 700

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amewaachia huru wafungwa 722 na kuwapunguzia vifungo wafungwa wengine 2,808 ambao wamebaki gerezani kumalizia kifungo kilichobaki.

Msamaha huo ulitolewa jana ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 55 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Taarifa ya msamaha na kupunguza vifungo ilitolewa jana na Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Meja Jenerali Jacob Kingu.

"Wafungwa 3,530 watafaidika na msamaha huu ambapo 722 wataachiwa huru leo (jana), wafungwa 2,808 watabaki gerezani kumalizia kifungo kilichobaki baada ya msamaha huu," alisema.

Alisema ni mategemeo ya serikali kuwa watu hao watarejea tena kwenye jamii na watajiepusha kutenda makosa ili wasirejee gerezani.

"Wafungwa wote wapunguziwe robo ya adhabu zao baada ya punguzo la kawaida la moja ya tatu linalotolewa chini ya kifungu cha Sheria ya Magereza Sura ya 58, wafungwa hao sharti wawe wametumikia robo ya adhabu zao gerezani isipokuwa walioorodheshwa katika Ibara ya 2(i-xxi)," Meja Jenerali Kingu alibainisha katika taarifa yake hiyo.

Meja Jenerali Kingu alisema wafungwa walioingia gerezani kabla ya Machi 15, mwaka huu wakiwa na magonjwa ya Kifua Kikuu (TB), Ukimwi na saratani ambao hali zao siyo nzuri, wathibitishwe na jopo la waganga chini ya uenyekiti wa waganga wakuu wa mikoa au waganga wakuu wa wilaya ili kunufaika na msamaha huo.

Alilitaja kundi lingine la kunufaika na msamaha huo kuwa ni wafungwa wa kike walioingia na mimba gerezani na wenye watoto wanaonyonya na wasionyonya.

"Wafungwa wenye ulemavu wa mwili na akili, ulemavu huo uthibitishwe na jopo la waganga chini ya uenyekiti wa waganga wakuu wa mikoa au waganga wakuu wa wilaya," alisema.

Katika taarifa yake hiyo, Katibu Mkuu huyo alibainisha kuwa msamaha huo hauwahusu wafungwa wenye adhabu ya kunyongwa au makosa ya kujaribu kuua, kujaribu kujiua au kuua watoto wachanga.

Alisema msamaha huo pia hauwahusu wafungwa waliohukumiwa kifungo cha maisha, wanaotumikia vifungo vya makosa ya kujihusisha na usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya kama cocaine, heroin na bangi.

Alisema msamaha huo pia hauwahusu wafungwa wanaotumikia kifungo cha makosa ya kujihusisha na uombaji, upokeaji au utoaji rushwa, wenye kifungo cha makosa ya unyang'anyi wa kutumia silaha au kujaribu kutenda makosa hayo.

"Wafungwa wanaotumikia kifungo cha makosa ya kupatikana na silaha, risasi au milipuko isivyo halali, wanaotumikia makosa ya wizi na ubadhirifu wa fedha za serikali, makosa ya kutoroka au kujaribu kutoroka chini ya ulinzi halali au kusaidia kutendeka kwa makosa hayo na bado wangali wanatumikia adhabu zao, msamaha huu hauwahusu," alisema.

Meja Jenerali Kingu alisema wafungwa ambao waliwahi kufungwa (warudiaji) na wale wenye makosa ya kinidhamu gerezani nao hawahusiki katika msamaha huo.

## HABARI ZA KITAIFA




Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dk. Titus Kamani (kushoto), akifungua mkutano wa siku mbili wa Jukwaa la Ushirika Mkoa wa Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ofisa ugavi mbaroni tuhuma wizi wa saruji

**Na Daniel Limbe,** CHATO

JESHI la Polisi wilayani Chato mkoani Geita, linamshikilia Ofisa Ugavi Msaidizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Benjamin Mugeta, kwa tuhuma za wizi wa saruji.

Takriban mifuko ya saruji 134 kati ya 600 iliyonunuliwa na halmashauri hiyo kwa ajili ya ujenzi wa madarasa ya Shule ya Sekondari Bwina inadaiwa kuibwa kabla ya kukabidhiwa kwa shule hiyo.

Inadaiwa ofisa ugavi huyo ndiye aliyesindikiza gari lililobeba saruji hiyo kabla ya kukabidhiwa kwa shule hiyo, lakini kamati ya ujenzi ikagoma kupokea mzigo huo kutokana na kuwa pungufu ya idadi ya mifuko iliyopaswa kupokewa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Mponjoli Mwabulambo, alidai kutokuwa na taarifa za tukio hilo licha ya kuahidi kufuatilia kwa wasaidizi wake.

"Sijapata taarifa za tukio hilo naomba nilifuatilie kujua ukweli wake tafadhali," alisema.

Hata hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Chato, Mtemi Msafiri, alisema ana taarifa za kuwapo kwa tuhuma hizo na kueleza kuwa wamezikabidhi kwa vyombo vya dola ili zifanye kazi.

"Ndiyo, taarifa tunazo, sisi ndiyo tulioagiza polisi wamkamate kwa mahojiano na hatua zingine za kisheria zichukuliwe kadri watakavyoona inafaa," alidai.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Bwina, Charles Abel, alidai kamati ya ujenzi haikupokea mzigo huo kutokana na upungufu uliojitokeza.

Alidai mifuko 600 ilipaswa kufika shuleni, lakini ilipelekwa 466, jambo ambalo waliona waliripoti kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.

"Mie nilitimiza wajibu wangu kwa kumfahamisha mwajiri ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri," alidai.

# Ripoti ya makusanyo yawatega wakurugenzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RIPOTI ya mapato ya ndani ya halmashauri kwa kipindi cha robo tatu ya mwaka wa fedha 2018/19, imewaweka mtegoni wakurugenzi wa halmashauri za majiji, manispaa, wilaya na miji waliokusanya chini ya asilimia 50.

Akitoa taarifa hiyo jana kwa waandishi wa habari jijini Dodoma, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, aliagiza mkurugenzi wa kila halmashauri kujitathmini, akibainisha kuwa ripoti hiyo ndiyo kipimo cha utendaji kazi.

"Kabla ya kufika robo ya mwisho, wakurugenzi ni kipindi cha kujitathmini sasa ni kwa namna gani anathamini kazi yake, kuhakikisha anaendelea kukusanya mapato," alisema.

Jafo pia aliwataka wakurugenzi kutowafumbia macho watendaji wa chini yao wanaohujumu mapato.

"Niwatake pia wakurugenzi hawa kukusanya mapato ni jambo moja na kutumia ni suala lingine kama tulivyoagiza asilimia 40 ya mapato haya iende kwenye miradi ya maendeleo," alisema.

"Mwisho wa mwaka tutazipima halmashauri hizi ambazo zilitakiwa asilimia 40 ya fedha hizo ziende kwenye miradi ya maendeleo, hawakupeleka kwenye miradi, hii ni hoja nyingine ambayo wakurugenzi wanapaswa kujitathmini."

Jafo alisema hataki kuzungumza litakalowapata, lakini wanapaswa kujitathmini na kutimiza wajibu wao.

DAR YAONGOZA

Waziri Jafo alisema Mkoa wa Dar es Salaam umeongoza kwa wingi wa mapato, ukiwa umekusanya Sh. bilioni 118.4, ukifuatwa na Dodoma Sh. bilioni 57.3, Mwanza Sh. bilioni 22.9, Arusha Sh. bilioni 22.8 na Mbeya Sh. bilioni 19.8.

Mikoa iliyoongoza kiasilimia ni Iringa asilimia 77, Geita asilimia 73, Dar es Salaam asilimia 72, Dodoma asilimia 68 na Songwe asilimia 68.

Alibainisha kuwa mikoa iliyofanya vibaya

INAENDELEA UK. 8

# TMA: Kimbunga kimebadili mwelekeo

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA) imewataka wananchi wa mikoa ya Mtwara na Lindi kuendelea na shughuli zao kama kawaida kwa sababu kimbunga ambacho kilitarajiwa kusababisha athari kwenye ukanda huo kimebadili mwelekeo.

Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, alitoa kauli hiyo jana na kueleza kuwa kimbunga hicho kimekwenda kusini zaidi mwa Pwani ya Msumbiji, lakini akatahadharisha kuwa bado kipo kwa kuwa kitarudi tena baharini.

"Kwa sasa, kimbunga bado kipo ardhi ya Msumbiji na mwishoni mwa wiki kinatarajia kurudi baharini kama tulivyoeleza awali kwa kitaalamu, tunaomba wananchi kwa sasa waendelee na shughuli zao huku wakiendelea kufuatilia utabiri wa TMA," alisema.

Dk. Kijazi alisema kimbunga hicho kitakaporejea baharini kama walivyoeleza awali, kitaleta athari ukanda huo wa kusini lakini wananchi wataarifiwa ili wachukue tahadhari.

Alisema kwa wakati huo aliokuwa anazungumza, hali ya hewa ya mikoa ya Lindi na Mtwara ilikuwa ya mawingu ambayo hayakuwa na athari.

"Maeneo ya Magharibi mwa Ziwa Viktoria kuna wingu zito limetanda. Tunawapongeza sana wananchi kwa kusali na kutii kwa kwenda maeneo maalum yaliyotengwa huku wasipate athari. Tunazishukuru mamlaka mbalimbali, zimeonyesha ushirikiano mkubwa kwenye suala hili," alisema.



# HakiElimu yaiangukia serikali bajeti ya elimu

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya HakiElimu imeiomba Serikali kuongeza bajeti ya sekta ya elimu ili kukidhi mahitaji ya ongezeko la wanafunzi wanaodahiliwa na utekelezaji wa elimu msingi bila ada.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu bajeti ya sekta ya elimu kwa mwaka wa fedha 2019/20, Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu Dk. John Kallaghe, alisema katika vipindi vitatu vilivyopita vya miaka ya fedha, bajeti ya elimu imekuwa ikishuka kwa takribani asilimia moja kila mwaka. Alisema mwaka 2016/17 bajeti ya elimu ilikuwa Sh. bilioni 4,770, lakini ilishuka hadi kufikia Sh. bilioni 4,706 na katika mwaka wa fedha 2017/18 na mwaka 2018/19 bajeti iliyoidhinishwa pia ilishuka zaidi hadi kufikia Sh. bilioni 4,628.

"Katika hali ya kawaida tungetegemea bajeti ya sekta ya elimu ingepanda ili kukidhi mahitaji ya ongezeko la wanafunzi wanaodahiliwa na utekelezaji wa elimu msingi bila ada. Uwiano kati ya bajeti ya sekta ya elimu na bajeti kuu ya serikali umeshuka na kupungua chini ya viwango vinavyokubalika kikanda na kimataifa," alisema Dk. Kallaghe.

Alisema uwiano wa bajeti ya elimu kwenye bajeti ya serikali umepungua kutoka asilimia 16.1 kwa mwaka 2016/17 hadi asilimia 15 kwa mwaka 2017/18 na kushuka zaidi hadi kufikia asilimia 14 kwa mwaka 2018/19.

"Kwa kuzingatia ongezeko la bajeti ya taifa katika miaka mitatu na kama serikali ingetenga angalau asilimia 20 kwa sekta ya elimu, bajeti ya sekta hii ingeongezeka kwa jumla ya Sh. bilioni 4,666, kiwango hiki kama kingepangwa na kutolewa kingepunguza kwa kiasi kikubwa changamoto za miundombinu ya elimu," alisema Dk. Kallaghe.

Pia, waliiomba serikali iangalie uwezekano wa kufanikisha upatikanaji wa taulo hizo moja kwa moja mashuleni kama ambavyo inafanyika katika baadhi ya nchi jirani.

"Kulingana na wizara ya elimu shule za msingi nchini zina upungufu wa walimu takribani 85,916 hadi kufikia mwezi Aprili mwaka jana. Mei 2 mwaka jana Serikali kupitia kwa Naibu Waziri wa Tamisemi, Joseph Kakunda, waliliambia Bunge kuwa hadi kufikia Juni 30, 2018 itakuwa imeajiri jumla ya walimu 10,140 wa shule za msingi ili kukabiliana na upungufu katika shule hizo. "Hata hivyo hadi kufikia mwezi Julai 2018 ni walimu 4,840 ambao walikuwa wamepangiwa shule za msingi na sekondari. Mwezi Februari mwaka huu serikali ilitangaza kuajiri takribani walimu 4,549 tu katika ngazi mbalimbali za elimu, hivyo kwa idadi hiyo ni dhahiri kuwa Serikali imeshindwa kufikia lengo la kuajiri walimu 10,140 wa shule za msingi," alisema.

Aidha, Dk. Kallaghe alisema pamoja na umuhimu wa upangaji wa bajeti, suala la utekelezaji wa bajeti inayoidhinishwa ni muhimu zaidi.




Mkuu wa mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo (wa pili kulia), akipokea moja ya vibao 200 vya kuongoza usalama barabarani vilivyotolewa na benki ya NMB katika Shule ya Msingi Sinoni jijini Arusha jana. Kutoka (kushoto) ni Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali wa NMB, Filbert Mponzi, Meneja wa Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro, Mkurugenzi wa Bodi ya NMB, Dk. George Mulamula na Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Jonathan Shanna. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Dk. Kusiluka mwenyekiti wa TASAF

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, amemteua Dk. Moses Kusiluka (pichani), kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Uongozi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi kupitia Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, Dk. Kusiluka ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu.

Taarifa hiyo iliwataja wajumbe wa Wajumbe wa Kamati ya Taifa ya Uongozi ya TASAF kuwa ni Balozi Zuhura Bundala, Dk. Dorothy Gwajima na Dk. Charles A. Mwamwaja.

Wajumbe wengine ni Dk. Ruth Rugwisha, Dk. Naftali B. Ng'ondi, Mhandisi Hussein Mativila na Richard Z. Shilambo.

Taarifa hiyo ya Balozi Kijazi ilieleza zaidi kuwa uteuzi huu ulianza Aprili 23, 2019.



# Maabara ya Polisi DNA sasa mbioni kusajiliwa kwa mkemia

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

JESHI la Polisi nchini, liko katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za kisheria ili maabara yake ya uchunguzi wa vinasaba (DNA), isajiliwe na Mkemia Mkuu wa Serikali na kuiwezesha kufanya kazi sambamba na maabara ya uchunguzi wa kikemia.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola alitoa taarifa hiyo juzi, alipowasilisha bungeni hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2019/20 ya Wizara hiyo.

"Jeshi la Polisi kwa mwaka 2019/20 litaongeza ufanisi katika utendaji wa maabara ya uchunguzi wa sayansi jinai kwa kuongeza vifaa vya kisasa na kutoa mafunzo ya kujengea uwezo askari wapelelezi ndani na nje ya nchi," alisema.

Aidha, Waziri Lugola alilieleza Bunge kuwa kuanzia mwaka mpya wa fedha 2019/20, Jeshi la Polisi kupitia Shirika lake la Uzalishaji Mali (TPFCS), litaanza kufanya mafunzo ya matumizi ya silaha za moto kwa kampuni binafsi za ulinzi, mashirika ya umma na wamiliki binafsi wa silaha. Alisema mpango huo ni matakwa ya sheria yanayolenga kuimarisha matumizi sahihi na ulinzi wa maeneo hayo.

"Natoa wito kwa wamiliki na watumiaji wote wa silaha za moto kushirikiana na Jeshi la Polisi kutekeleza matakwa haya ya kisheria," alisema. Alisema katika kipindi cha Julai 2018 hadi kufikia Machi mwaka huu, jumla ya makosa makubwa ya jinai 45,574 yaliripotiwa katika vituo vya Polisi nchini ikilinganishwa na makosa 47,236 yaliyotokea katika kipindi kama hicho mwaka 2017/2018. "Kupungua kwa makosa hayo kumetokana na kupatikana mapema taarifa za uhalifu kwa kutumia askari wa intelijensia, ushirikishwaji wa wananchi kupitia Polisi jamii katika udhibiti wa uhalifu nchini; kuimarika kwa doria, misako na operesheni maalum mijini, vijijini na majini; na ushirikiano na vyombo vingine vya dola," alisema Lugola

Kuhusu makosa ya barabarani na ajali, Waziri Lugola alisema makosa ya barabarani yamepungua kwa asilimia 38 na vifo vitokanavyo na ajali za barabarani kwa asilimia 38.7

Pamoja na mambo mengine, Waziri Lugola alisema katika mwaka 2018/19 kuwa jumla ya askari 130 wa vyeo mbalimbali, maafisa 28, wakaguzi 14 na sakari 88 wamechukuliwa hatua za kinidhamu na za kisheria, baada ya kubainika kujihusisha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili mema ya Jeshi la Polisi.

"Aidha, maafisa wawili, wakaguzi saba na askari 88 walishtakiwa kijeshi, askari 35 walipewa adhabu ya kufukuzwa kazi, askari watatu walifikishwa mahakamani na askari wawili walishushwa vyeo. Maafisa 25 na wakaguzi wanne waliandikiwa barua za onyo, kujieleza na tahadhari."

## NECTA yatahadharisha udanganyifu kidato 6

**Na Happy Severine,** MASWA

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA), Dk. Charles Msonde amewataka wanafunzi wa kidato cha sita nchini, wanaotarajia kufanya mtihani wao wa mwisho mwezi ujao, kuepuka udanganyifu.

Pamoja na hayo ameupongeza mkoa wa Simiyu kwa ubunifu wake wa kuanzisha kambi za kitaaluma zinazopelekea mkoa huo kupiga hatua kubwa kielimu kwa kushika nafasi za juu kitaifa ukilinganishwa na awali.

Dk. Msonda alisema hayo jana wakati akizungumza na wanafunzi wa kidato cha sita waliopo kwenye kambi ya kitaaluma iliyopo shule ya sekondari Maswa Girls wilayani Maswa.

Alisema ameamua kutembelea kambi hiyo ili kuwaondoa hofu na homa ya mtihani kwa wanafunzi hao ili waweze kufanya vizuri zaidi na waachane na fikra za kutaka kufanya udanganyifu.

"Ninachowasihi wanangu, watahiniwa wote ...tena wa nchi nzima kuepuka homa ya mtihani ambayo itawasababishia kushindwa kufanya vema mitihani yenu," alisema. Dk. Msonde aliongeza kuwa ni vema wakayasoma kwa umakini maswali na kujibu kwa kujiamini kwa kurejea kile walichofundishwa kuliko kujaribu kufanya udanganyifu.

Nae Afisa elimu Mkoa wa Simiyu, Ernest Hinju, alisema awali mkoa ulikuwa na ufaulu mbaya, lakini kupitia kambi za kitaaluma zilizoanzishwa mkoani humo ufaulu umepanda kwa kiasi kuanzia matokeo ya kidato cha nne na sita.

"Mwaka 2017 kabla ya kambi matokeo ya kidato cha sita tulikuwa nafasi ya 26 yaani ya mwisho kitaifa ...baada ya kambi matokeo ya mwaka 2018 tulishika nafasi ya 10, kidato cha nne mwaka 2017 kabla ya kambi tulishika nafasi ya 11 baada ya kambi tulishika nafasi ya 9 kitaifa kwa hali hii kambi zina tija," alisema.

Katika hatua nyingine wanafunzi waliopo kambini hapo walisema kuwa ujio wa Katibu Mtendaji huyo wa NECTA umekuwa chachu ya ufaulu wao na kuahidi kuyafanyia kazi yale yote aliyoyaeleza ikiwamo kuepuka udanganyifu pamoja na kuondoa homa ya mtihani.



Mwendesha guta akiwa amelisheheni mzigo na abiria juu katika Barabara ya Uhuru, eneo la Ilala TBL, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Magufuli aikumbuka shule yake kwa mchele, ng'ombe

**Na Rose Jacob,** MWANZA

RAIS John Magufuli, jana alitoa ng'ombe watano wenye thamani ya Sh. milioni mbili na kilo 500 za mchele zenye thamani ya Sh.milioni moja kwa wanafunzi zaidi 554 wa kidato cha sita katika shule ya sekondari Sengerema.

Rais Magufuli alitoa motisha hiyo kupitia kwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, ambaye aliwakilishwa na Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Emanuel Kipole ambaye alikabidhi vyakula hivyo kwa Mkuu wa Shule hiyo, Zakaria Kahema, mbele ya wanafunzi hao. Akizungumza katika makabidhiano ya zawadi hiyo katika shule hiyo, Kipolea aliwataka wanafunzi hao kuhakikisha wanafanya vizuri katika mitihani yao ya kumaliza kidato cha sita na kuhakikisha hatotokea kati yao atakayepata sifuri, kwa kuwa Rais Magufuli amewaboreshea mazingira ya shule yao.

"Rais wa awamu ya tano John Magufuli hii shule ya sekondari Sengerema ndio kituo chake cha kwanza cha kufundishia, hivyo mtambue umuhimu alionao kwenu na mfanye vizuri katika mitihani yenu shule iweze kushika nafasi nzuri katika kumi bora, hii mtakuwa mmemfariji sana Rais wetu," alisema Kipole kwa niaba ya Mongella.

Naye Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani Sengerema, Mark Makoye, alitoa kilo 100 za mchele kwa niaba ya chama hicho, huku akiwataka wanafunzi hao kutambua juhudi za CCM inayoongozwa na Rais Magufuli kuwa hatokubali kuona wanafunzi wanataabika katika suala zima la kupata elimu.

Naye mkuu wa shule hiyo, Kahema, alisema tangu Serikali ya Awamu ya Tano ingie madarakani na kuboresha mazingira ya elimu, shule hiyo imeongeza ufaulu na mwaka jana.

"Sisi kama watumishi wa shule hii tutamuenzi Rais wetu kwa kufanya kazi kwa uadilifu kama yeye anavyofanya na wanafunzi hawa wanayo shahuku kubwa ya kufanya vizuri ili wasimvunje moyo wa kuweza kuiamini shule yetu na shule zingine," alisema Kahema.

Nao wanafunzi wa shule hiyo walimshukuru Rais kwa kuwaganyia mambo mazuri ambayo yanawatia moyo na kuiona serikali iko pamoja nao, huku wakimuombea kwa Mungu azidi kumlinda na kumtia nguvu ya kuliongoza Taifa.

# Ndugai ataja mambo 4 ya usindikaji mazao

**Na Frank Monyo**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ametaja hatua nne za kuchukua kwa ajili ya maendeleo ya biashara zitokanazo na mazao ya kilimo na viwanda vitokanavyo na usindikaji mazao hayo.

Alitoa kauli hiyo hivi karibuni alipokuwa akifungua mhadhara wa umma kuhusu mwelekeo wa upatikanaji wa chakula, kukuza mnyororo wa thamani wa bidhaa zitokanazo na kilimo duniani ambao uliendeshwa na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), ulioenda sambamba na uzinduzi wa Shahada ya Sayansi ya Uchumi na Fedha itakayotolewa na chuo hicho.

Ndugai ambaye alikuwa mgeni rasmi , alizitaja hatua hizo kuwa ni serikali lazima iendelee kuweka mazingira mazuri ya sera ambazo zitawafanya wafanyabiashara wadogo na wa kati na viwanda vinavyosindika mazao ya kilimo kukua na kustawi.

"Pili, wazalishaji wadogo wanahitaji msaada kuwawezesha kushindana katika soko la ndani, kikanda na kimataifa, kwa mfano mafunzo yanaweza kusaidia kuboresha stadi zao za usimamizi mzuri wa shughuli zao. Hili IFM mnaweza kusaidia kutoa elimu na stadi za biashara katika kilimo," alisema.Nyingine ni upatikanaji dhaifu wa huduma za fedha kwa muda mrefu zimedumaza maendeleo vijijini nchini.

Ndugai alitaja hatua ya nne ni uwekezaji katika utafiti wa kilimo ni muhimu ili kuibua teknolojia mpya katika kilimo ambazo zinaweza kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Hata hivyo, alisema rasilimali fedha za kutosha zinapaswa kuelekezwa katika utafiti mbalimbali wa kilimo ili kuhakikisha wakulima wadogo wanaweza kukabiliana na mabadiliko hayo kwa kutumia mbegu bora.

Naye Mkuu wa Chuo cha IFM, Prof. Tadeo Satta, alisema chuo kimeona umuhimu wa kuendesha mihadhara kwa umma ili kutoa elimu stahiki na kusaidia Serikali katika kukuza sekta ya viwanda na uchumi.

Alisema chuo kuongeza shahada hiyo ina lengo la kulisaidia taifa kuwa na wataalamu wa elimu ya juu hasa katika fani ya uchumi na fedha ambayo pia ni sekta muhimu kwa nchi. Kwa sasa IFM inaendesha kozi zaidi ya 35 katika fani mbalimbali.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachambuzi wa soka wekeni ushabiki kando

**MSIMU** wa Ligi Kuu Bara 2018/19, unaelekea ukingoni wakati huu timu 20 zinazoshiriki ligi hiyo isipokuwa Simba pekee, zikiwa zimebakiza mechi tano hadi sita kabla ya pazi la msimu huu kufungwa rasmi.

Yanga ambayo imebakiza mechi sita kabla ya kumalizika kwa ligi hiyo msimu huu, ndiyo iliyopo kileleni ikiwa na alama 74 ikifuatiwa na Simba yenye pointi 66 sawa na Azam iliyoko nafasi ya tatu ikiwa imeshuka dimbani mara 32, lakini Wekundu wa Msimbazi hao wenyewe wakicheza mechi 26 tu hadi sasa.

Simba ambayo leo itashuka dimbani ugenini mjini Musoma kucheza mechi yao ya 27 dhidi ya Biashara United, imekuwa nyuma ya ratiba kutokana na awali kukabiliwa na mechi za kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo iliishia hatua ya robo fainali kwa kutolewa na TP Mazembe kwa jumla ya mabao 4-1.

Hata hivyo, suala la waamuzi kutofuata sheria 17 za soka ama kwa kutofahamu au pengine kwa kurubuniwa ili kutotenda haki, limekuwa likilalamikiwa kila mara msimu huu.

Baadhi ya mashabiki wamefika mbali hadi kuelekeza kuvurunda kwa waamuzi hao kwamba ni mpango mkakati wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), kutaka kuzibeba baadhi ya timu.

Ni ukweli usiopingika kwamba kuna baadhi ya waamuzi wamekuwa wakivurunda katika maamuzi yao wanapochezesha mechi, lakini pia tukiwa kama wadau wakubwa wa soka nchini, tunachelea kukubali ama kuona tuhuma hizo zikielekezwa TFF kwa madai ya kutaka kuzibeba baadhi ya timu.

Cha kushangaza ni kwamba wanaoituhumu TFF wanakwenda mbali zaidi kwa kuainisha ushabiki ama mapenzi ya kila kiongozi wa shirikisho hilo na klabu yake.

Haya yote yanatokana na Simba kuwa na viporo vingi, na inaposhinda ama mwamuzi kufanya hata makosa ya kibinadamu katika maamuzi yake, moja kwa moja viongozi wa TFF wamekuwa wakihusishwa jambo ambalo Nipashe tunaona si sahihi kwa maendeleo ya soka letu.

Na mbaya zaidi baadhi ya wachambuzi wa soka, watangazaji wa vipindi vya micheza na wasemaji wa klabu, ambao Nipashe tulitarajia kuona wakiwa mstari wa mbele kuchambua kwa weledi na umakini zaidi kwa kutumia sheria 17 za soka, wamekuwa wapotoshaji wakubwa ama kwa kutofahamu au kutokana na kubebwa na mapenzi ya klabu wanazozishabikia.

Na kwa kufanya kwao hivyo, kumekuwa kukiongeza chuki kwa TFF na kufanya wanachama wake ambao ni klabu, wadau na mashabiki wa soka nchini kulichukia shirikisho hilo kama si kukosa imani nalo kabisa.

Cha muhimu tunaona ipo haja kwa makocha na viongozi wa klabu kujifunza kukubali matokeo badala ya kila timu zao zinapopoteza kuelekeza kilio chao kwa waamuzi na TFF kwa kudai wanazibeba baadhi ya timu.

Mpira wa miguu una matokeo matatu, kushinda kushindwa na kutoka sare, na unapofurahia ushindi pia ukubaliane na siku ya kulia unapopoteza, na si kila timu yako inapofanya vibaya uigeukie TFF na waamuzi.

Ikumbukwe pia waamuzi nao ni binadamu na ndiyo maana kwa sasa baadhi ya ligi hususan Ulaya zimekuwa zikitumia teknolojia ya video kumsaidia refa (VAR), huku kwingineko wakitumia wasaidizi wa nne, wawili; pembeni na pembeni na wawili kila moja nyuma ya goli, lengo likiwa ni kumsaidia refa na kumwezesha kubaini makosa ambayo anashindwa kuyanasa kwa macho yake.

Hivyo, wakati huu TFF ikijitahidi kuipeleka Ligi Kuu walipo wenzetu ambao wamepiga hatua, wachambuzi wa soka hawana budi kuwa makini katika uchambuzi wao na kuweka ushabiki kando ili kusaidia soka letu kukua kwa kutoka hapa lilipo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# TFF amkeni, lisemwalo lipo, kama halipo linakuja

Na Barnabas Maro

**JAMBO** linalosemwa huwa tayari limeshatokea au kama sivyo karibuni litatokea. Methali hii hutumiwa kumnasihi mtu mwenye tabia ya kuyapuuza mambo anayoambiwa na watu wengine kwa kuyaona kama upuuzi au uvumi tu. Yafaa kuyazingatia.

Ni mpaka tutakapopata viongozi wasio na U-simba au U-yanga kwenye Shirikisho la Kandanda nchini (TFF), ndipo kanuni na sheria zitakapofuatwa na kutekelezwa ipasavyo. Vinginevyo ni ubabaishaji tu. Kama Shirikisho hilo likiendeshwa na viongozi wenye mwelekeo wa Simba au Yanga, basi uamuzi utakaotolewa ni kuzinufaisha klabu hizo.

Kwa nini? "Kipendacho moyo ni dawa" maana yake anachokipenda mtu au inachokipenda roho ya mtu huwa ni kama dawa yake. Methali hii hutumiwa kumpigia mfano anayeelekea kukipenda kitu fulani sana ingawa wengine wanakiona kuwa kibaya.

"Msema kweli hakosi." Maana yake mtu asemaye ukweli hakosi, alisemalo huwa. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kwamba aghalabu mtu mwenye tabia ya kusema ukweli huishia kuaminiwa na watu wengine. Ni vizuri tuwe na tabia ya kuusema ukweli ndipo tuaminiwe.

'Uongozi' ni madaraka anayopewa mtu ya kusimamia au kuongoza shughuli. Madaraka anayopewa mtu hayatumiki kuunufaisha upande mmoja hata kama amefanya jambo kinyume cha utaratibu na sheria ili kuukandamiza mwingine, bali atakiwa kutenda na kuamua haki.

Tumeona mara nyingi Simba na Yanga zinaposhiriki mashindano ya kimataifa hupewa muda mwingi sana na kushiriki Ligi Kuu ya Bara hata kuwa na viporo 10 na kuendelea. Hata huko Ulaya utaratibu wa aina hii upo kwani timu zinazoshiriki mashindano ya kimataifa huwa nyuma kwa mechi mbili au moja tu kwenye ligi yao.

Lakini timu zetu zinaposhiriki michezo ya kimataifa huwa na viporo vingi na ili kwenda sawa na wenzao waliocheza mechi nyingi ligi ya nyumbani hucheza baada ya takriban siku tatu au nne .

Hali hii yaweza kusababisha timu kununua mchezo kwa timu ambazo hata zikishinda haziwezi kutwaa ubingwa au kushika nafasi za juu na hata kuepuka kushushwa daraja. Hapa ndipo viongozi wa TFF wanapotakiwa kutenda haki hata kama ni wanachama au mashabiki wa Simba na Yanga. Kuna mara nyingi marefarii hufanya mambo ya ajabu viwanjani, lakini hakuna hatua thabiti wanazochukuliwa.

Wakati mwingine rushwa hupewa wachezaji hatari wa mbele na nyuma ili wasifunge au kufanya makosa yatakayosababisha timu kufungwa. Kinachofanyika ni wachezaji wa aina hiyo kuahidiwa kusajiliwa na timu inayogawa rushwa.

Je, kumsajili mchezaji mpenda rushwa hawezi kufanya hivyo atakapopewa hela ili kusababisha timu yake ishindwe na yeye kutia noti kibindoni? Kuna maana gani ya kumsajili mchezaji kama huyo anayejali hela kuliko klabu anayoichezea? Wachezaji wenye tamaa ya hela wanapaswa kufungiwa kabisa na kuwapa nafasi wenye uchungu wa timu zao waendelee.

Mbali na wachezaji, pia kumekuwa na habari za chini chini kuwa hata marefarii hupewa rushwa ili kuzipendelea Simba na Yanga. Tetesi kama hizi zapaswa kufanyiwa kazi na atakayegundulika afutwe kabisa kwenye urefarii na jina lake litumwe Fifa. Hata timu zingine (ziitwazo ndogo ingawa hakuna ndogo kwenye michuano ya Ligi Kuu Bara) zinapotoa malalamiko yao kwa TFF mara nyingi malalamiko yao huishia hewani kwa kuzinufaisha Simba na Yanga!

**Uchaguzi wa Yanga**

Kuna baadhi ya wanaogombea nafasi za uongozi Klabu ya Yanga majina yao yaliondoshwa kwa kushindwa kuweka sawa hesabu za mapato na matumizi walipokuwa viongozi. Ilivyo ni kwamba mambo yameishia hapo! Watu wameshindwa kueleza jinsi fedha za Yanga zilivyotumiwa kwa njia halali wanaachwa vivi hivi bila kuwakabidhi kwa wapelelezi wa Takukuru ili watakaohusika na ubadhirifu wafikishwe mbele ya sheria?

Kuna baadhi ya wagombea wanataka nafasi za uongozi si kwa manufaa ya klabu bali kwa manufaa yao. Kwanza kutafuna fedha za klabu ili wajinufaishe na pili kujitafutia umaarufu ili kugombea ubunge. Yanga isifanye ngazi ya kuwavusha waroho wa madaraka na tamaa ya fedha ili kuwanufaisha. Walioshindwa kujibu maswali ya matumizi ya fedha za klabu waripotiwe Takukuru ili ukweli ufichuliwe.

Klabu ya Yanga ina mabilionea wengi wenye uchungu nayo, lakini wanashindwa kutoa hela kwa wasiwasi wa kuliwa na viongozi wasio waaminifu. Kama Yanga itakuwa na viongozi wenye uchungu na klabu, nawafahamu baadhi ya mabilionea walio tayari kuisaidia Yanga kwa hali (utendaji) na mali (fedha).

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

HABARI KITAIFA




Wakala wa Tigo Pesa Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, Justin Mbazi (kulia), akipokea mfano wa hundi ya Sh. milioni mbili, kutoka kwa Meneja Mauzo Tigo Kilimanjaro, Tryphone Kamugisha, baada ya kuvuka malengo waliyopewa Mawakala Kanda ya Kaskazini kupitia Promosheni 'Cash In' iliyomalizika mwishoni mwa Machi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Malima kuunda timu kuchunguza ushirika

**Na Timothy Itembe**, TARIME

MKUU wa mkoa Mara, Adamu Kigoma Malima, ameahidi kuunda timu ya kuchunguza mwenendo mzima wa utekelezaji wa shughuli za Chama cha wakulima wa Mara (WAMACU) ili wakulima wawe na imani na chama chao pindi majibu yatakapo toka.

Timu hiyo inatarajia kufanyakazi ndani ya miezi miwili na kutoa majibu kwenye mkutano mkuu wa WAMACU unaotarajiwa kufanyika Julai, mwaka huu.

Malima aliamua kuunda timu hiyo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya viongozi wa vyama vya msingi vya ushirika wa mazao mkoani Mara ambao walihudhuria kikao cha kupokea taarifa ya ukusanyaji na uuzwaji wa kahawa wa msimu 2018/2019 kilichofanika mjini hapa.

Malima alisema kuwa Serikali imelenga kufufua ushirika wenye nguvu na wenye tija na kwa hali hiyo kama mkuu wa mkoa wa Mara aliyeteuliwa na Raisi John Magufuli kumwakilisha, atahakikisha anatekeleza na kusimamia malengo ya serikali.

"Kama mnataka kuwa na WAMACU ya siku zote, mimi sina matatizo, lakini nataka muwe na WAMACU mpya yenye tija ambayo ina viongozi ambao ni wabunifu wenye lengo la kuongeza uzalishaji wa kahawa ili wakulima wakaondokane umaskini," alisema na kuongeza:

"Na kama kuna changamoto inayowakumba viongozi wa WAMACU nitaunda timu ya kuchunguza hizo changamoto na itatoa majibu mwezi wa saba kwenye mkutano kama huu ambao nitaenda kuugharimia mimi."

Mwenyekiti wa Amcos Nkongore, James Makoromu, alimuomba Malima awasaidie wakulima kwa kuwa wanaumia kutokana na fedha za malipo ya kahawa wanayolipwa na WAMACU kutokueleweka.

Alisema kuwa malipo ya awali walikubaliana kulipwa Sh. 1,000 ili kusubiri malipo, lakini malipo yao yamecheleweshwa bila sababu za msingi.

# Wizara yashauriwa juhudi zaidi kuboresha elimu

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WIZARA Elimu, Sayansi na Teknolojia, imetakiwa kuongeza juhudi za kuboresha elimu ya msingi na sekondari nchini, ili kufanikisha azma ya serikali ya kuingia uchumi wa kati kupitia viwanda.

Ushauri huo ulitolewa na mwakilishi wa mkuu wa mkoa wa Mwanza, Dk. Philis Nyimbi, ambaye ni mkuu wa wilaya ya Nyamagana wakati akifungua mkutano wa 26 wa baraza la wafanyakazi wa wizara hiyo jijini hapa.

Mkutano huo ulihudhuliwa na wajumbe zaidi ya 90 kutoka vitengo na idara za wizara hiyo, kwa ajili ya kujadili maboresho yanayofanywa na serikali pamoja na wadau mbalimbali wa sekta hiyo nchini.

"Misingi iliyowekwa na serikali ya awamu ya tano ya upatikanaji wa elimu bora nchini, suala hilo liko mikononi mwa watendaji walio katika idara mbalimbali za wizara ya elimu hivyo," alisema.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. James Mdoe, alisema serikali imewekeza fedha nyingi katika uboreshaji wa miundombinu kuanzia elimu ya msingi hadi vyuoni, ili kuhakikisha wanafunzi wanapata elimu bora inayokidhi matakwa ya sera elimu nchini.

"Tumekutana hapa Mwaza ili kupitia utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kipindi cha mwaka 2018 /2019, kujadili mwelekeo wa bajeti kwa mwaka 2019/2020 kabla ya kuwasilishwa bungeni," alisema Mdoe.

Kwa upande wake, Katibu wa baraza hilo, Graceana Shirima, alisema: "Menejimenti imekuwa ikifanya kazi za sekta ya elimu kwa kushirikiana na vyama vya wafanyakazi ikiwamo TUGHE na CWT kwa kipindi cha miaka mitatu ya uhai wa baraza hili katika kufanikisha masuala mbalimbali za wizara hiyo," alisema.

# Watetezi haki binadamu sasa waja kivingine

**Na Salome Kitomari**

MTANDAO wa Watetezi wa haki za Binadamu Tanzania (THRDC), unawafundisha watetezi kutumia mitandao ya kijamii na digital kufikisha ujumbe wa kupinga uvunjifu wa haki za binadamu.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo yaliyoanza jana jijini Dar es Salaam, Afisa kujenga uwezo wa THRDC, Doegratius Bwire, alisema mafunzo hayo yamejumuisha taasisi mbalimbali katika kuelekea kilele cha maadhimisho ya siku ya watetezi wa haki za binadamu.

"Tumebaini matumizi ya mitandao ya kijamii kwa watetezi wa haki za binadamu ni madogo sana, tunawafundisha namna gani wataitumia kupaza sauti bila kuvunja sheria zilizopo na kufikisha ujumbe kwa watawala," alisema.

Alisema nchi kama India ambayo imeendelea kwenye matumzi ya digital, watetezi wa haki za binadamu wanajua namna ya kutumia mitandao ya kijamii kupaza sauti dhidi ya uonevu wowote unaojitokeza.

"Tunaweza kuwa na harakati fulani mtandaoni tukipinga utawala usiozingia sheria na haki za binadamu, kwa kutumia mitandao tukafikisha ujumbe na kufanya mijadala ya kina ya kukabiliana na mambo mbalimbali," alisema.

Bwire alisema matumizi ya mitandao ya kijamii kwenye kusukuma mabadiliko ni geni kwa Tanzania, na kwamba ni muhimu sana hasa kipindi cha uchaguzi mkuu ambako watetezi hujikuta katika mazingira magumu.

Alisema kwa kutumia msukumo huo watawala ambao hawaheshimu utawala wa sheria watаogopa na kubadili mwelekeo katika kuheshimu sheria zilizopo nchini.

Aidha, alisema kesho (Jumapili) itakuwa ni kelele cha maadhimisho ya siku ya watetezi wa haki za binadamu, na Azaki zitashiriki chini ya kaulimbiu ya nafasi ya Azaki kwenye utetezi wa haki za binadamu mitandaoni.

# JPM aingilia kati usajili laini za simu

INATOKA UK. 2

ndugu zangu, mimi ndiyo mtumishi wenu kwa sababu wananchi Mbeya mkiwamo wamachinga, mlinifanya niwe kiongozi wenu na sasa mnahitaji eneo la biashara ambako ni mjini, watu wanaotaka kufanya Nanenane wakafanye na hili eneo la uwanja wa ndege mmelipata," alisema.

Rais Magufuli aliuagiza uongozi wa mkoa huo kuhakikisha eneo hilo linakuwa la wafanyabiashara wadogo na kutaka wapewe vitambulisho ili wasibughudhiwe.

"Wamachinga tunalibadilisha eneo hilo matumizi leo ambayo ni siku ya Muungano wa Tanzania tumetimiza miaka 55.

Liandaliwe vizuri litakuwa la wamachinga Mbeya," Rais Magufuli alisema na kuwataka wafanyabiashara wadogo wasikubali kutumiwa na wafanyabishara wakubwa ili kukwepa kodi.

Aliupongeza Mkoa wa Mbeya ambao awali ulikabidhiwa vitambulisho vya wajasiriamali wadogo 25,000 vikamalizika na awamu ya pili wamepewa vitambulisho 80,000 na hadi sasa wameshaviuza 36,000.

Rais Magufuli pia alizungumzia kiwanda cha nyama ambacho kilijengwa enzi za uongozi wa Mwalimu Julius Nyerere lakini sasa kimetelekezwa, akiiagiza Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha kinafufuliwa.

Rais Magufuli pia aliutaka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ujielekeze kujenga majengo viwanda vya dawa na vifaa vya hospitali.

Pia aliwataka Watanzania kuendelee kuwaenzi waasisi wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

"Leo (jana) ni maadhimisho ya miaka 55 ya Muungano wa Tanzania, hatujafanya sherehe lakini naomba tuwaenzi Mwalimu Nyerere na Karume kwa kazi kubwa waliyofanya," alisema.

Rais Magufuli alimpongeza Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' (Chadema) ambaye tangu juzi alipoingia mkoani humo, alikuwa pamoja naye.

"Mbunge Sugu naye alisugua kuanzia uwanja wa ndege hadi nilikokwenda nikaona ndiyo mweleko wa kuelekea CCM, haya yote ni mapenzi ya utanzania, hii ndiyo Tanzania yetu iliyoachwa na Rais Karume na Baba wa Taifa Nyerere ya kujenga umoja wa Watanzania," alisema.

Rais Magufuli anaendelea na ziara yake mkoani Mbeya, leo akitarajiwa kuzindua barabara ya Mbeya - Chunya yenye urefu wa Km 72.

**AAGIZA UCHUNGUZI MTOTO ANAYEDAIWA KULAWITIWA**

Katika hatua nyingine, Rais Magufuli aliwaagiza Makamanda wa Polisi Mikoa ya Songwe na Mbeya kufanya uchunguzi upya wa madai ya kuwapo kwa tukio la mtoto mwenye umri wa miaka minne kulawitiwa na mzee mwenye umri wa miaka 53.

Rais Magufuli alitoa agizo hilo jana kwenye Viwanja vya Ruanda Nzovwe jijini Mbeya katika ziara yake ya siku nane mkoani humo baada ya mama aliyejitambulisha kuwa Swaumu Satimaninjenje kueleza kero yake.

Mama huyo aliyedai ni mkazi wa Songwe mkoani Mbeya, alidai mbele ya Rais kuwa mtoto wake wa kiume huyo alilawitiwa lakini hadi sasa hajapata haki licha ya kwenda hadi kwa Jaji Mkuu na Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini kueleza kuhusu tukio hilo.

"Mheshimiwa Rais, mtoto wangu alilawitiwa, nimefika hadi kwa IGP (Mkuu wa Jeshi la Polisi) na Jaji Mkuu, nimehama nyumbani kwangu kutoka Tunduma, polisi wananiweka ndani viongozi wa kitaifa wakija ili nisikutane nao nieleze tatizo hili," mama huyo alidai mbele ya Rais Magufuli.

Swaumu alidai ana watoto watatu na mmoja kati yao ndiye aliyelawitiwa lakini kesi ilipoanza, akaambiwa mtoto wake ana miaka 20, jambo ambalo si la kweli.

"Nimelalamika kote, nilipeleka malalamiko kwa Jaji Mkuu akasema mambo yangu yashughulikiwe, hawakushughulika, IGP alimpigia simu RPC wa Momba, wakasema hawajamkamata mtuhumiwa," mama huyo alidai.

Baada ya maelezo hayo, Rais Magufuli alimwagiza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya kuanza uchunguzi wa tukio hilo upya ili mama huyo apate haki.

"RPC wa Mbeya mfikishie taarifa RPC wa Songwe mshughulikie suala hili, muanze uchunguzi upya halafu mniletee taarifa, msaidizi wangu wa sheria chukua taarifa za huyu mama na nyaraka," Rais Magufuli aliagiza.

Alisema nyaraka zote za kesi hiyo zichukuliwe na kutolewa nakala na kumwagiza RPC kuhakikisha mama huyo hasumbuliwi na analindwa.

Rais Magufuli alimkabidhi mama huyo Sh. milioni moja kwa ajili ya matunzo ya mtoto huyo baada ya awali mama huyo kudai ana hali ngumu kimaisha na mtoto wake aliyedai kulawitiwa amepata matatizo makubwa kiasi cha kushindwa kuzuia haja kubwa.

**Imeandikwa na Nebart Msokwa (MBEYA) na Romana Mallya (DAR)**



Katibu wa Chama cha Wazazi wenye Watoto wa Kichwa Kikubwa na Mgongo Wazi (Asbaht), Mkoa wa Dar es Salaam, Milton Byemerwa, akisisitiza jambo katika kikao na baadhi ya wanachama wa chama hicho, mapema wiki hii. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ripoti ya makusanyo yawatega wakurugenzi

INATOKA UK. 3

Manyara ambao umekusanya Sh. bilioni 6.5, Lindi Sh. bilioni 6.1, Rukwa Sh. bilioni 5.8, Kigoma Sh. bilioni 4.5 na Katavi Sh. bilioni 3.8.

"Mikoa mitano ya mwisho kwa kigezo cha asilimia ni Shinyanga asilimia 46, Katavi asilimia 43, Kigoma asilimia 42, Lindi asilimia 42 na Mtwara asilimia 26," alisema.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam nayo imeongoza kwa kigezo cha asilimia kwa kukusanya asilimia 87 ya makisio huku Jiji la Tanga likishika nafasi ya mwisho kwa kukusanya asilimia 57 ya makisikio.

Kwa upande wa majiji, Jafo alisema Jiji la Dodoma limeendelea kuongoza kwa kigezo cha wingi wa mapato kwa kukusanya Sh. bilioni 50 huku Jiji la Tanga likiwa la mwisho kwa kukusanya Sh. bilioni 8.7.

Jafo alizitaja halmashauri zilizoongoza kwa kigezo cha asilimia kuwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi iliyokusanywa kwa asilimia 113 ya makisio, Geita asilimia 109, Wanging'ombe asilimia 105, Kilolo asilimia 103 na Sumbawanga asilimia 92.

Halmashauri za mwisho

Alizitaja halmashauri tano za mwisho kwa kigezo cha wingi wa mapato kuwa ni Wilaya ya Madaba iliyokusanya Sh. milioni 293.7, Wilaya ya Newala Sh. milioni 268.3, Kakonko Sh. milioni 238.6, Buhigwe Sh. milioni 177.3 na Momba Sh. milioni 170.4.

Jafo alisema Manispaa ya Sumbawanga imeongoza kwa kundi la manispaa kiasilimia, ikiwa imekusanya kwa asilimia 92 huku Lindi ikishika nafasi ya mwisho kwa kukusanya asilimia 23.

## Mbunge ahoji vijana kujiajiri katika uchumi wa viwanda

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Kaliua (CUF), Magdalena Sakaya, ameihoji serikali ina mpango gani wa kuwasaidia vijana wanaokosa nafasi wapate ujuzi ili kujiajiri kuelekea uchumi wa viwanda.

Akiuliza swali la nyongeza bungeni mwishoni mwa wiki, Sakaya alihoji serikali ina mpango gani kujenga chuo cha Veta Kaliua ili vijana wanaomaliza masomo na kukosa nafasi wamweze kupata mafunzo yatakayowawezesha kujiajiri ili kuendana na kaulimbiu ya uchumi wa viwanda.

Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, William Ole Nasha, alisema azma ya serikali ni kujenga vyuo hivyo kila wilaya na mikoa.

Aidha, katika swali la msingi Mbunge wa Ulanga (CCM), Goodluck Mlinga, alisema wilaya ya Ulanga ina shule za msingi zaidi ya 50 na zaidi ya 17 za sekondari lakini haina chuo chochote ambacho hao wanafunzi wanaomaliza masomo kwenye shule hizo wanaweza kujiunga nacho. "Je, Serikali inasema nini juu ya hali kama hiyo?,"alihoji

Akijibu swali hilo, Ole Nasha alisema Serikali inatambua umuhimu wa vyuo hivyo katika uandaa rasilimali watu itakayochangia katika kufikia azma ya Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati ifikapo 2025. Alisema kwa sasa serikali inatekeleza mpango wa kuboresha vyuo vilivyopo kwa kukarabati na kujenga miundombinu mipya pamoja na kuongeza vifaa vya kisasa vya kufundisha na kujifunzia ili kuongeza nafasi za udahili na kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo yatolewayo.

Aidha, serikali inatekeleza mpango wa ujenzi wa vyuo vya Veta za mkoa na wilaya kutegemeana na upatikanaji wa fedha,

Alibainisha kuwa Wilaya ya Ulanga ni pamoja na wilaya zenye uhitaji mkubwa wa vyuo vya elimu ya mafunzo.

Alisema wilaya ina chuo kimoja cha ufundi stadi cha Mtakatifu Francis kinachomilikiwa na sekta binafsi.

HABARI KITAIFA

# Euro milioni 37 za ruzuku ya EU zatumika usalama baharini EAC

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

JUMUIYA ya Afrika Mashariki (EAC) kwa kushirikiana na Shirikisho la Maendeleo Pembe ya Afrika (IGAD) pamoja na Tume ya Bahari ya Hindi (IOC), wametekeleza mkakati wa usalama baharini kwa kiasi cha Euro milioni 37.5 zilizotolewa na rukuzu za Umoja wa Ulaya ( EU).

Hayo yalibainishwa katika taarifa ya EAC kupitia vyombo vya habari na kusema miongoni mwa hatua zinazozingatiwa chini ya mpango huo ulioanza kwa miaka mitatu, ni kuzidisha uwezo wa mamlaka zinazochunguza uhalifu za nchi washiriki kufanya hivyo ipasavyo na kwa ukamilifu wakichunguza uhalifu kwenye bahari kwa msingi wa sheria timilifu.

EAC ilipewa jukumu katika suala hilo na ilianza kwa kuendesha mafunzo ya wachunguzi wakiangazia uchunguzi jumuishi, ikiwamo na teknolojia na tathmini ya uhalifu, vipindi sita vya mafunzo vikihusisha maafisa 50 katika kila kundi yalifanyika kati ya miezi ya Januari na Juni 2018.

Maafisa hao walishiriki katika mafunzo ngazi ya juu kwa kila kundi wakiangazia tathmini ya uhalifu katika kipindi cha Aprili 23, mwaka huu nchini Mauritius na kumalizika Mei 5, 2019.

Hata hivyo mafunzo yanafanyika katika Chuo cha Magereza cha Mauritius Mjini Port Louis, Shirika la Polisi la Kimataifa (INTERPOL), kwa mujibu wa Mkataba na EAC wa 2012.

Mafunzo hayo yalizinduliwa rasmi na Mkuu wa Sheria ambaye pia ni Waziri wa Masuala ya Sheria, Haki za binadamu na Marekebisho ya Katiba wa Mauritius, Maneesh Gobin, ambaye alisisitiza haja ya utendaji kazi wa pamoja, miongoni mwa mataifa ya kanda katika kukabiliana na mitandao ya uhalifu kati ya mipaka ya nchi.

Alieleza kutokana na kuongezeka kwa uhamiaji wa watu, uhamishaji wa bidhaa na fedha, kiwango cha uhalifu wa hali ya juu kimeshamiri kwa kuwa kuna ushirikiano wa juu kiuchumi na kibiashara, hivyo alishauri kuendelea kuboresha kiwango cha ubadilishanaji wa taarifa baina ya vyombo vya usalama. Pia alisisitiza suala la kuimarisha malengo ya pamoja na ikiwezekana kupanua mpango wa mafunzo, ili kuhusisha mataifa zaidi kama yale ya visiwani yanayotumia lugha ya Kifaransa, ambayo mifumo yake ya sheria ni tofauti ili hali usalama ni suala nyeti kwa mataifa ya pwani na baharini na yale ya bara.

Washiriki walitoka Burundi, Kenya, Rwanda, Somalia, Seychelles, Mauritius, Sudan Kusini, Tanzania na Uganda.




Mchuuzi wa mihogo ya kukaanga, akifanya biashara katika mazingira hatarishi kiafya katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Vijana duniani kujadili afya Morogoro

**Na Gwamaka Alipipi**

VIJANA 200 kutoka mataifa mbalimbali duniani, wanatarajia kukusanyika mjini Morogoro kwenye Mkutano Mkuu wa Kimataifa wa Baraza Kivuli la Vijana la Umoja wa Mataifa (TIMUN), kujadiliana kuhusu afya ya uzazi na umuhimu wa kutunza amani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mratibu Mkuu wa Mkutano huo, Kelvin Edward, alisema mbali na mada hizo vijana watajadiliana pia kuhusu ushiriki wao katika kutunza mazingira, nafasi yao katika ushirikishwaji kwenye masuala ya ajira.

Alisema mkutano huo utaanza Aprili 29 hadi Mei 3, mwaka huu, ambapo vijana kutoka mataifa zaidi ya 200 watakusanyika na kujadiliana.

"Vijana kutoka nchi mbalimbali Afrika na Ulaya watakusanyika kwenye mkutano wa TIMUN, lengo kuu ni kuwainua vijana na kuwashirikisha kwenye maendeleo endelevu, ujio wa vijana hao nchini itakuwa ni fursa kiuchumi,"alisema Edward.

Aliongeza kuwa kwenye mkutano huo vijana watapata fursa ya kujua kazi zinazofanywa na mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN). Pia watajifunza masuala ya uongozi na diplomasia.

Alisema maadhimio yatakayopatikana katika mkutano huo yatawasilishwa makao makuu ya UN na kufanyiwa kazi.

"Vijana watajifunza namna gani ya kutunza amani ama washiriki vipi katika kuitunza amani, mrejesho wa mawazo katika mkutano huo utawasilishwa katika idara ya vijana UN Tanzania," alisema Edward.

Akizungumza kwa niaba ya mwakilishi mkazi wa UN, Afisa Habari, Didi Nafisa, alisema UN itaendelea kuwasaidia vijana kujihusisha na malengo endelevu ya milenia.

"Vijana wanamchango mkubwa katika ongezeko la watu, wanapaswa kuelezwa kuwa wanamchango katika kufanikisha maendeleo endelevu ya milenia hususani nyakati hizi ambazo wanaelekea katika kupata matokeo chanya," alisema Nafisa.

Naye Mwenyekiti wa Asasi ya Vijana UN (Yuna), Jolson Msaki, alisema mkutano wa TIMUN unawaleta karibu vijana na UN na kwamba mkutano huo ni wa 22 kufanyika ambapo unafadhiliwa na UN Tanzania, Ofisi ya Waziri Mkuu, Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Watoto (Unicef) na Ubalozi wa Marekani.

## Elimu yawabadili wanawake wafugaji

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

WANAWAKE wa jamii ya kifugaji katika Tarafa ya Enduiment wilayani Longido, wamepokea mabadiliko chanya kwa kupatiwa elimu na Shirika la Maendeleo ya Jamii ya Afrika Mashariki la Oikos na kuachana na mila kandamizi.

Kabla ya kupatiwa elimu hiyo, walikuwa wanakubali kuachiwa majukumu ya kifamilia na waume zao.

Yambaine Saying'o, mkazi wa Kata ya Kitendeni, alisema miaka ya nyuma walikuwa wakiachiwa majukumu ya kujenga nyumba pamoja na kulisha familia, huku kipato chao kikiwa duni.

Alisema wengi walikuwa wakienda kwenye vibarua kwa ajili ya kuchimba viazi Ili walipwe na kupata viazi kidogo kwa ajili ya chakula, huku waume zao wakiishia kulewa pombe.

"Unakwenda kufanya vibarua, ukichimba viazi ukajaza gunia unalipwa Sh. 5,000 bado mzee akija anataka akute chakula, kwa kweli tunaishukuru shirika La Oikos kutupatia elimu ya ujasiriamali," alisema.

Aidha, alisema shirika hilo limewapatia elimu ya ujasiriamali juu ya uzalishaji bidhaa pamoja na kuuza ikiwa ni sehemu ya wao kujikwamua katika umaskini.

" Kupitia elimu tuliyopatiwa sasa tuna uwezo wa kufanya biashara ndogo ndogo tukapata fedha, tukajiunga katika makundi na tukakopeshana kupitia biashara zetu, watoto wetu tunawasomesha na wanapata chakula na huduma ya afya," aliiambia Nipashe.

Mratibu wa mradi wa CONNEKT, Samantha Button, alisema mradi huo unatekelezwa na Shirika la Oikos chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU) katika eneo la Enduiment wilayani Longido (Tanzania) na Ambuseli upande wa Kenya. Alisema kuwa mradi huo umebeba matawi mengi ikiwamo kumuinua mwanamke kiuchumi kwa kumpatia elimu ya ujasiriamali, na hadi sasa wanawake zaidi ya 300 katika Tarafa ya Enduiment, Kata ya Sinya na Kamwanga wamepatiwa elimu hiyo..

Alieleza pia EU imeshawapatia Euro zaidi ya milioni moja na ambazo zimeutekeleza mradi huo.

Samantha alisema mbali na mafunzo hayo pia wametoa sola kwenye hifadhi ya EWMA, wanafunzi wa shule za msingi Olmolog na Lerangwa na kuwapatia elimu juu ya uhifadhi wa mazingira na kugharamia mafunzo ya askari jamii 40 wa hifadhi ya EWMA.

Alidai wanatarajia kuanzisha kiwanda cha kuchakata ngozi kati ya Kata ya Sinya au Tinga Tinga ambacho kitawasaidia wakazi wa eneo hilo hususan katika kipindi hiki cha athari za mabadiliko ya tabianchi.

# Wawakilishi wa wazazi shuleni watimuliwa kikaoni

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MWENYEKITI wa bodi ya Shule ya Msingi Pasua Manispaa ya Moshi, Shaban Machivya, amewatoa wawakilishi vijana kwenye kikao cha wazazi kwa kile kilichodaiwa kushindwa kuchangia mijadala na changamoto zinazowakabili wanafunzi hao.

Alifanya hivyo juzi kwenye kikao cha wazazi na walezi cha kujadili maendeleo ya wanafunzi na nidhamu shuleni.

Alisema amelazimika kuwatoa wawakilishi hao vijana kwenye kikao kwa kuwa wamekuwa wakishindwa kuchangia hoja na kushindwa kufanya maamuzi juu ya hatima ya wanafunzi kitaaluma na kinidhamu.

"Wazazi wamekuwa na kasumba ya kuwatuma wawakilishi ambao wakifika hapa wanashindwa maamuzi ya wanafunzi wanaosoma hapo, wakati mwengine wazazi wanapokuja kushirikisha hukataa maazimio yaliyopitishwa na kikao hicho," alisema na kuongeza:

"Tunapiga marufuku tabia hii ya kutuma wawakilishi kufika kwa ajili ya maendeleo ya watoto, huku nyinyi mkienda kwenye shughuli zenu za kiuchumi ... tunawaomba wazazi kuangalia misingi ya hawa watoto na kutoa ushirikiano wa hali ya juu kwa walimu ili tuweze kufikia lengo la kujenga kizazi imara."

Mratibu wa Elimu Kata ya Bomambuzi, Ermelinda Kyara, alikiri kuwapo kwa changamoto kwenye vikao kutokana na ushiriki mdogo wa wazazi kwa mambo muhimu yanayowahusu wanafunzi yakiwamo chakula nidhamu na maendeleo kwa ujumla.

Alisema ikiwa mzazi hana dharura ya msingi, ni vyema akafika kwenye vikao ili kueleza changamoto zinazomkabili.

"Watoto hawa wanahitaji ushirikiano wa kutosha kati ya wazazi, walezi na walimu katika kuwajengea misingi imara. Tulijadili suala la chakula mashuleni, lakini wazazi hawajalipa hadi leo na wanapokumbusha hudai ya kuwa hawana taarifa... hii ni mbaya na sisi kama viongozi hatutakubali jambo hili liendelee tena," alisema.

Baadhi ya wazazi akiwamo Neema Mfinanga, walipongeza uamuzi uliofanywa na mwenyekiti wa bodi na kusema hali hiyo imekuwa ikiwarudisha nyumba katika kuchangia misingi ya maendeleo na nidhamu kwa watoto wao.

Aidha waliomba serikali kupitia Wizara ya Elimu kuangalia suala la wazazi wasio na dharura za msingi kutuma wawakilishi wasioweza kufanya maamuzi ya hatma ya watoto wao.

"Ikiwa kuna uwezekano ziundwe sheria ndogo zitakazowadhibiti wazazi wanaokaidi wito wa kufika na kusikiliza hatima ya watoto wao kwa sababu imebainika wao ndio chanzo kikuu cha matukio ya kikatili kwa watoto," alisema Zulfa Mohamed.



Msaidizi wa Mbunge wa Musoma Vijijini, Fedson Masawa (kulia), akikabidhi vitabu 1,000 vya masomo mbalimbali kwa Mwalimu wa Shule ya Msingi Imam Shafii ya Musoma Mjini, Omary Yandiro, vilivyotolewa na mbunge huyo, Prof. Sospeter Muhongo (hayupo pichani), katika hafla iliyofanyika shuleni hapo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC atishwa migogoro mashamba ya kahawa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SERIKALI imesema inakabiliwa na mgogoro mkubwa na wawekezaji wa mashamba makubwa ya vyama vya ushirika vilivyokuwa vikijihusisha na kulima kahawa na viongozi waliokula mali za vyama vya ushirika.

Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, ndite aliyetoa kauli hiyo alipokuwa akizungumza na Nipashe jinsi mgogoro huo unavyoweza kuathiri amani ya mkoa na kupunguza uzalishaji.

Alisema serikali imefanya jitihada za kila namna kuwakamata na kuwashtaki wawekezaji 'feki' katika mashamba makubwa ya kilimo cha kahawa kwa muda mrefu bila mafanikio, hivyo kuamua kuanzisha kamati itakayosaidia kutafutwa kwa amani mkoani hapa.

Alisema wakazi wa mkoa wa Kilimanjaro hawanabudi kuamka na kukimbia mchaka mchaka katika masuala ya uchumi kwa kuwa hata zao hilo limekuwa likiachiwa wazee, hali ambayo imepunguza uzalishaji.

Alisema ipo haja ya kuunda jumuiya ya maridhiano itakayohakikisha inaelimisha jamii katika kuondoa migogoro iliyopo kwenye vyama vya ushirika badala yake kuwapo ushirika ambao ndio sehemu salama ya kuhakikisha elimu ya kilimo cha kisasa inapatikana.

"Ikiwa tutafanya hivyo tutaweza kuzuia migogoro ya wakulima na wafugaji, mipaka kati ya mikoa na mikoa, wilaya na wilaya na nchi na nchi ili wananchi waweze kushiriki kupiga vita viendo vya kuuhujumu uchumi, biashara za magendo na dawa za kulevya mipakani," alisema.

James Silayo, mwanachama wa chama cha ushirika Uru, alisema uwapo wa migogoro kwenye vyama vya ushirika na ubadhirifu kumesababisha kuporomoka kwa zao hilo nchini.

Naye mkoboaji wa kahawa, Erinest Mushi kutoka Kibosho Umbwe, alisema kwa sasa wateja wa kukoboa zao hilo wamepungua kwa asilimia kubwa kutokana na kukatishwa tamaa na migogoro katika vyama vya ushirika.

# Marufuku viongozi usuluhishi kesi mimba

**Na Mary Mosha,** SAME

WILAYA ya Same imepiga marufuku tabia ya baadhi ya viongozi wa makundi ya kijamii, vitongoji na vijiji kujadili na kusuluhisha kesi zinazohusiana na wanafunzi kupewa ujauzito ama kuolewa katika umri mdogo.

Aidha serikali imelitaka Jeshi la Polisi na Mahakama kutenda haki katika kushughulikia mashauri yanayohusu masuala hayo kwa kuepuka vitendo vya rushwa, bali sheria ifuate mkondo wake.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema hayo wakati akifungua kikao cha wadau wa masuala ya jinsia, haki za mtoto wa kike iliyoandaliwa na shirika la World Vision kwa lengo la kupambana na mimba na ndoa za ututoni nchini.

Alisema kitendo cha kufanya usuluhishi kwa masuala ambayo yanahitaji mkondo wa kisheria, huku wazazi ma walezi wakipewa fedha kama fidia ni kumnyima mtoto wa kike haki yake ya msingi ya kupata elimu na kutimiza ndoto zake maishani.

Senyamule alisema katika hali isiyo ya kawaida, zaidi ya wanafunzi 95 wa shule za msingi na sekondari wamepewa mimba kwa kipindi cha miezi sita wilayani Same, jambo lililosababisha kukatishwa masomo yao.

Kwa upande wake, mratibu wa masuala ya jinsia, utetezi na kampeni kutoka shirika la World vision, Jesca Ndang'a, alisema kampeni hiyo itafanyika kwa miaka mitano kuunga mkono serkali kupinga ndoa za ututoni pamoja na kutimiza malengo ya maendeleo endelevu husan elimu. Alisema katika kampeni hiyo watazielimisha familia na jamii kwa ujumla kuepuka vitendo vya ukatili na kuwapa watoto husussan wa kike fursa ya kupata elimu.

Kwa upande wao, baadhi ya wadau Ezekel Idrisa na Christina Mmanda wametaka serikali, viongozi wa dini na wanaharakati kwa ujumla kuongeza kasi katika kuielimisha jamii kuhusu athari za mila na utamaduni zilizopitwa na wakati ambazo zinaruhusu ndoa za ututoni.





Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Deogratius Ndejembi, akizungumza wakati wa kukabidhiwa miradi wa maendeleo iliyokuwa ikitekelezwa na Shirika la World Vision Tanzania, katika hafla iliyofanyika kwenye Kijiji cha Sanzawa, wilayani humo, mkoani Dodoma juzi.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali sasa yaombwa bajeti ya kutosha maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kuhakikisha inatenga fedha za kutosha katika sekta ya maji kutokana na bajeti yake kupungua kwa asilimia 26.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mwenyekiti wa Mtandao wa Maji na Usafi wa Mazingira Tanzania (TAWASANET), Mhandisi Herbert Kashililah, katika kongamano la miaka 10 ya Shirika lisilo la kiserikali la Shahidi wa Maji ambalo lilishirikisha wadau wa maji ikiwamo wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Mifugo jijini hapa.

Alisema Mtandao huo umeangalia kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2006 hadi mwaka wa fedha 2018/19 na kubaini fedha zinazotengwa kwenye sekta hiyo zinapungua kwa asilimia 26.

"Hii inatokana na wakati mwingine fedha zinatengwa na kuidhinishwa na bunge, lakini kiasi kinachotolewa ni kidogo au wakati mwingine zinachelewa hata kutekeleza miradi ya maji," alisema.

Akizungumzia uchafuzi wa maji mijini, Kashililah alisema kuna changamoto ya uchafuzi wa maji kutokana na viwanda kutililisha maji kwenye mito kama mto Msimbazi.

"Sisi Tanzania tuna sheria na sera nzuri sana, lakini nini kinafanyika kudhibiti uchafuzi mengi ambayo tumeona kwamba Watanzania hawajali na pia mamlaka ya uwajibikaji ni mdogo kutokana na kutokuwa na rasilimali za kutosha kudhibiti hali hiyo," alisema.

Akizungumzia uhakika wa maji kwenye miji inayokua, alisema wameangalia katika Jiji la Dar es Salaam wananchi waliohojiwa wamesema kuna tatizo kubwa la maji kwa asilimia 49 huku Morogoro kwa asilimia 77. Aidha, alisema asilimia 63 ya kaya Dar es Salaam zinasema kuna changamoto ya usafi wa mazingira.

"Pia ubora wa maji ni tatizo kwenye maeneo mengi," alisema.

Kwa upande wake, Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Devotha Minja, alisema kuna miradi mingi imetekelezwa kutokana na kutengwa kwa fedha kwenye mfuko wa maji na kuahidi kuwa wataendelea kuhimiza serikali kutenga fedha kwenye sekta hiyo.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Bunge, Dk. Christine Ishengoma, alisema watahimiza serikali kuongeza fedha kwa sekta ya maji ili kuhakikisha kunakuwapo na upatikanaji wa maji.

"Tunaomba fedha zinazotengwa zitoke zote kwa kuwa wakati mwingine fedha zinatengwa, lakini hazitoki zote, tunaishauri na kuiomba serikali kuhakikisha fedha zote zinazotengwa zitolewe zote maji ni uhai," alisema.

Awali, akizungumzia dhumuni la kongamano hilo, Meneja Mradi wa Shirika la Shahidi wa Maji, Pendo Hyera, alisema wameandaa kongamano hilo ili kusaidia kuondokana na changamoto zinazokabili sekta ya maji.

"Ni muhimu kujadili usimamizi na upatikanaji wa rasilimali maji, tuhakikishe kuna upatikanaji wa maji kwenye kukuza viwanda, na Shirika hili liliona liadhimishe miaka 10 tangu kuanzishwa kwake kwa kufanya kongamano linalohusisha wadau ili kuishauri serikali," alisema.

# Mabilioni yaja kufikisha huduma ya mawasiliano

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MFUKO wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), umesema Mei mwaka huu unatarajia kutangaza zabuni ya kufikisha huduma za mawasiliano katika kata 214 zenye vijiji 521 itakayogharimu Sh. bilioni 26.5.

Hayo yalibainishwa jana na Mtendaji Mkuu wa mfuko huo, Mhandisi Peter Ulanga, katika maadhimisho ya miaka 10 ya Mfuko huo yatakayozinduliwa leo na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alieleza kuwa ifikapo Mei mwaka huu watatangaza zabuni ya kufikisha huduma za mawasiliano katika kata na vijiji hivyo ambapo utekelezaji utaanza mara moja baada ya tathmini kukamilika mwishoni mwa Juni mwaka huu.

"Bado kuna maeneo ambayo hayana huduma za mawasiliano ambapo mfuko huo umejikita kuhakikisha yanapata huduma muhimu na Mei mwaka huu mfuko utatangaza zabuni ya kufikisha huduma za mawasiliano katika kata 214, zenye vijiji 521," alisema.

Aidha alisema serikali itatenga fedha kwa ajili ya maandalizi ya zabuni nyingine yenye vijiji zaidi ya 500 itakayotangazwa katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa gharama ya Sh. bilioni 26.

Ulanga alisema kiasi cha Sh. bilioni 118 kimetumika kufikisha mawasiliano tangu kuanzishwa kwake mwaka 2009 ndani ya kipindi cha miaka 10.

Alisema serikali kupitia mfuko huo imeshafikisha huduma za mawasiliano katika kata 703, zenye vijiji 2,501 na wakazi zaidi ya milioni tano kote nchini.

Alifafanua kuwa mchango huo wa serikali ni wastani wa asilimia 26 ya gharama za ujenzi na uendeshaji wakati watoa huduma wamechangia asilimia 74 kufanikisha uwekezaji huo.

Alibainisha toka kuanzishwa kwa mfuko huo umejikita kutambua mahitaji ya mawasiliano nchi nzima, kushirikiana na wadau mbalimbali wa mawasiliano nchini, kushirikisha wananchi katika kutambua na kutatua kero za mawasiliano.

"Wakati mfuko huu unaanza takribani asilimia 45 tu ya Watanzania walikuwa wanaishi katika maeneo yaliyofikiwa na mawasiliano ya simu, mpaka tunavyoongea leo takribani asilimia 94 ya Watanzania wanaishi kwenye maeneo yanayofikiwa na mawasiliano ya simu ambapo zaidi ya asilimia 70 ni watumiaji wa huduma hizo huku asilimia 10 imechangiwa na mfuko," alisema.

Kadhalika, alisema hadi sasa mfuko umepeleka vifaa vya Tehama katika shule zaidi ya 500 ambapo kila shule ilipata kompyuta tano na printa moja kwa wastani.

# Jiji lagawa viwanja 2005 maeneo ya migogoro

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imefanikiwa kugawa viwanja 2005 kwa ajili ya kumaliza tatizo la migogoro wa ardhi kwenye kata mbalimbali ambayo ilidumu kwa takribani miaka 40.

Akizungumza katika Baraza la Madiwani katika kikao cha kawaida cha kujadili utekelezaji wao kwa mwaka wa fedha 2018 -2019, Mkurugenzi wa Jiji hilo Godwin Kunambi, alisema changamoto kubwa kwenye sekta ya ardhi ni uelewa mdogo wa wananchi na pia migogoro mingi ilikuwapo tangu ilivyokuwapo Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu(CDA).

"Mwanzoni wakati tunakabidhiwa shughuli za ardhi katika jiji la Dodoma wananchi walidhani tutashindwa na tutaleta siasa, lakini tumeweza na katika kipindi cha mwaka mmoja na miezi minne tumepima viwanja 100,000 ambapo CDA kwa kipindi cha miaka 45 waliweza kupima viwanja 69,000 tu hakika tumeweza," Alisema Kunambi.

Diwani wa Ipagala Dotto Gombo aliwataka viongozi jiji hilo kufanya kazi kwa bidii na kuweka tofauti zao pembeni ili wasikwamishe maendeleo.

Hata hivyo aliwataka wataalamu wa kupima ardhi kutatua changamoto za wananchi kwa wakati.

"Unakuta sehemu kuna mgogoro wa ardhi wakiitwa idara ya upimaji kutatua mgogoro huo utasikia anasema kwamba tutakujia huko kuangalia badala ya kufafanua kwamba hilo eneo aidha ni la shule, barabara au misitu wawaambie nasio kumumunya maneno," alisema diwani huyo.

Naye, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Vijana), Anthony Mavunde, alisema jiji hilo limeingia katika historia kutokana na kufanikiwa kutatua mgogoro wa ardhi.

Mavunde alisema moja ya mikakati yake katika kampeni zake ni kutatua migogoro na wananchi wauziwe viwanja kwa bei rahisi jambo ambalo limefanikiwa.





# Aagiza wanaojipanga kwa rushwa uchaguzi wa 2020 wakamatwe

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, ameitaka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (Zaeca) kuwakamata na kuwafikisha katika vyombo vya sheria wale wote wanaojihusisha na rushwa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Amesema imezoeleka katika mchakato wa uchaguzi watu kujihusisha na rushwa, hivyo ni jukumu la mamlaka hiyo kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

Waziri Haroun aliyasema hayo alipokabidhi tuzo za washindi wa habari zinazohusiana na rushwa katika hafla iliyofanyika mjini Zanzibar.

Alisema ni wakati sasa Zanzibar kuiga mfano wa nchi ya China ambayo haina uvumilivu na watu wanaojihusisha na rushwa.

"Wenzetu China wana 'zero tolerance' (uvumilivu sifuri) kwa watu wanaojihusisha na rushwa, na hayo ndiyo mambo ya kuiga," Waziri Haroun alisema.

Aliwataka waandishi wa habari kuandika habari zitakazofichua vitendo vya rushwa vinavyoisumbua jamii. Alisema waandishi wa habari wana mchango mkubwa katika kutoa elimu kwa jamii kupambana na rushwa kwa kutumia taaluma yao.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Yakuti Hassan Yakuti, alisema kwa sasa taarifa za rushwa zinapewa umuhimu katika vyombo vya habari, hivyo ni vyema waandishi wakaendeleza kuziandika kwa kina zaidi.

Awali akitoa taarifa kuhusiana na tuzo hizo, Mkurugenzi wa Zaeca, Mussa Haji, alisema ofisi yake huzipa umuhimu wa kipekee na kuzifanyia kazi taarifa za rushwa zinazotoka katika vyombo vya habari.

Waandishi sita kutoka visiwani Zanzibar walipata zawadi mbalimbali katika mashindano ya uandishi wa habari zinazohusu rushwa.



Askari wa Usalama Barabarani, akilisimamisha moja ya magari kwa ajili ya ukaguzi wa kawaida katika barabara ya Mandela, eneo la Tabata Relini, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Mikakati ya kutokomeza malaria

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Afya Zanzibar, Harusi Said Suleiman, amesema wizara yake itaendelea kutumia mikakati ya kupambana na malaria ambayo imeonyesha mafanikio makubwa ya kupunguza maradhi hayo ili kuhakikisha ugonjwa huo unatokomezwa.

Ameitaja mikakati hiyo kuwa ni pamoja na kutumia vyandarua vilivyotiwa dawa, kutumia tiba ya dawa mchanganyiko, kufanya ufuatiliaji wa wagonjwa nyumbani na kuendelea na upuliziaji wa dawa majumbani katika sehemu ambazo bado wagonjwa wa maradhi hayo wanapatikana.

Naibu waziri huyo aliyasema hayo katika maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani yaliyofanyika katika Uwanja wa Misuka, Mahonda Wilaya ya Kaskazini B Unguja.

Alisema Zanzibar imepiga hatua kubwa katika kupambana na malaria hadi kufikia chini ya asilimia moja, lakini bado kuna baadhi ya sehemu hasa katika Wilaya ya Kaskazini B, Wilaya ya Kati na Wilaya ya Magharibi maradhi hayo yapo.

Alisema mafanikio hayo yamepatikana kutokana na juhudi kubwa zinazochukuliwa na serikali ikishirikiana na wadau mbalimbali kutokomeza ugonjwa huo.

Aliwataka wananchi waliopata vyandarua waendelee kuvitumia kikamilifu na kuvitunza, akieleza kuwa taarifa za ufuatiliaji wagonjwa majumbani unaonyesha kuwa matumizi ya vyandarua kwa jamii bado yapo chini.

Alisema Wizara ya Afya itaendelea kutoa vyandarua bila malipo kupitia vituo vya afya kwa mama wajawazito, watoto wenye umri wa miezi tisa na jamii kwa jumla.

Alisema huduma za uchunguzi wa malaria zinapatikana katika vituo vyote vya afya, vikiwamo vituo vya bandarini na uwanja wa ndege ambavyo vimewekwa kwa ajili ya wasafiri wanaoingia na kutoka Zanzibar.

Akizungumzia hali ya malaria katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, Katibu Tawala Wilaya Kaskazini B, Makame Machano, alibainisha kuwa kati ya watu 52,356 waliochunguzwa mwaka jana, 655 walibainika kuwa na vimelea vya malaria na wengi wanatoka Wilaya ya Kaskazini B.

Alisema tatizo la malaria katika mkoa huo linachangiwa na kuwapo kwa mazalia ya mbu, mwamko mdogo wa wananchi katika kutumia vyandarua vilivyotiwa dawa na wageni wanaoingia kutoka nje ya visiwa vya Zanzibar.

# Mbinu ya kukomesha uvuvi haramu yatajwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Kaskazini B Unguja, Rajab Ali Rajab, amesema vita dhidi ya uvuvi haramu itafanikiwa iwapo vyombo vya sheria vitakuwa tayari kushirikiana na Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) na kamati za uvuvi.

Amesema iwapo wahusika wa vitendo hivyo wataonewa huruma pindi wanapokamatwa bila ya kuchukuliwa hatua stahiki, vitendo hivyo vitaendelea kujitokeza na kuathiri uchumi wa taifa.

Alitoa kauli hiyo kwenye Ufukwe wa Kiwengwa baada ya kupokea taarifa kutoka Kikosi cha KMKM kilichokuwa kinafanya doria ya kawaida na kufanikiwa kukamata wavuvi ambao walikuwa wanatumia vifaa visivyoruhusiwa.

Alisema uongozi wa wilaya kwa kushirikiana na kikosi hicho utahakikisha hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi ya wote waliokamatwa wakidaiwa kujihusisha na shughuli za uvuvi haramu.

Alimwagiza Sheha wa Kiwengwa na Ofisa Uvuvi wa Wilaya hiyo kuiangalia kwa kina sheria ya uvuvi juu ya watu wanaoanzisha kambi kwa ajili ya uvuvi ili kujua muda sahihi wanaotakiwa kuweka kambi na muda wa kumalizika ili kuzuia vitendo hivyo kuendelea kujitokeza.

Mjumbe wa Kamati ya Uvuvi, Kiwengwa, Mudathir Ali, alisema kamati yao ya uvuvi imekuwa ikitoa taaluma juu ya athari za uvuvi haramu kwa wavuvi hao, lakini cha kushangaza bado vitendo hivyo vinaendelea kujitokeza mara kwa mara.

Wavuvi 11 wamekamatwa na kufikishwa katika Kituo cha Polisi Kiwengwa wakituhumiwa kujihusisha na uvuvi haramu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI APRILI 27, 2019



**ALICIOS AVUTIWA NA MUZIKI WA BONGO**

Soma UK.19



# Komaa nao watakuelewa tu Shamsa

BASI SAWA



## We JK Comedian ya kweli hayo?

MCHEKESHAJI anayeigiza sauti za viongozi mbalimbali, JK Comedian amedai kwamba katika fani hiyo hana mpinzani bali waliopo ni kama wanamsindikiza tu.

"Niko vizuri katika fani hii, hao wengine wanajaribu tu, sikuweka ndani vyeti vyangu kwa ajili ya kuremba bali kufanya kweli, kwa hiyo sibahatishi," amesema.

Amesema kwa sasa jina lake ni kubwa na amekuwa akipata tenda ya kushiriki kwenye matangazo mbalimbali ya biashara kwa kuwa anaimudu kazi yake.



## Kamua Msaga Sumu hawakuwezi

MKALI wa muziki wa singeli, Msaga Sumu ameamua kuwapotezea wasanii chipukizi wa muziki huo ambao wamekuwa wakitafuta malumbano kwake.

"Nimegundua kwamba wanatafuta kiki ili nao watoke, sasa nimeamua kuwapotezea, sitawajibu kama zamani kwani lengo lao ni kutaka wawe juu kupitia kwangu," amesema Msaga Sumu.

Msaga Sumu amesema muziki wa singeli hauwezi kutajwa bila kuwapo jina lake kwa kuwa ndiye mwanzilishi wake aliyeuwezesha kuwa juu.



## Eti Baraka da Prince unasema..!

MSANII Baraka Da Prince, amesema hataki kuulizwa habari za mchumba wake Najma, kwa madai kwamba ana mambo mengi anayotakiwa kuulizwa na siyo hilo.

"Anayetaka kujua habari zake amtafute atazipata, siyo kwangu, ninajua tu kwamba yuko kwa wazazi wake Uingereza, zaidi ya hapo sitaki kuulizwa habari hizo," amesema Baraka.

Baraka amesema yeye ni msanii wa muziki wa kizazi kipya, hivyo ingependeza kama angeulizwa maswali kuhusu kazi mpya alizonazo na siyo uhusiano wake na Najma.

"Ninajua maswali kuhusu Najma ni ya kunichokonoa tu lakini sitaki kabisa kumzungumzia, kwa kifupi ni kwamba anayetaka habari zake amuulize mwenyewe," amesema.

INSTA-TWITTER






Siku ukiwa unataka kuondoka kwenye hii dunia tuambie kabla hujaondoka ili wakina sie tujue la kufanya ukiwa haupo
**-Mose Iyobo.**



Neno "Nakupenda" ni kauli tu na sio swali, ila watu wengi wakishakutamkia wanasubiria jibu. Ni Kwanini ?
**- Nandy.**



# Komaa nao watakuelewa tu Shamsa

NYOTA wa filamu nchini, Shamsa Ford, ameonyesha kukerwa na tabia ya baadhi ya wasanii ya kupenda kuandika matusi kwenye mitandao ya kijamii na kuwataka wamuhofie Mungu.

Amesema msanii ni kioo cha jamii, na kwamba anapoandika matusi kwenye mitandao ya kijamii au kujianika ni sawa na kushindwa kujua wajibu wake mbele ya jamii inayomzunguka.

"Niwashauri wasipoteze muda kwa kufanya mambo ya ovyo, badala yake wamrudie Mungu wao ili mwisho wa siku wapate thawabu kuliko kukera wengine," amesema Shamsa.




>>> **Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

UNASEMAAA...

## Hapo hujakosea Siboka

MWIMBAJI wa nyimbo za asili, Costa Siboka amesema atajitahidi kutunga nyimbo kwa lugha za makabila mbalimbali nchini ili kujiongezea mashabiki.

Amesema amekuwa akitunga nyimbo kwa kutumia lugha za baadhi ya makabila ya kanda ya ziwa Victoria na kumfanya awe na mashabiki wa maeneo hayo tu.

"Ninataka sasa nipanue wigo wa kazi zangu ili kupata mashabiki wengi, hivyo niko mbioni kutunga nyimbo kwa kutumia lugha za makabila mbalimbali ya hapa nchini," amesema Siboka.



## Punguza ujiko Ebitoke

MCHEKESHAJI aliyejizolea umaarufu, Ebitoke amejipigia debe kuwa ubunifu wake katika sanaa ni wa kipekee na haujawahi kubuniwa na msanii mwingine nchini

"Niliangalia kila ubunifu ukiwamo wa kuigiza kama mtu mshamba nikagundua kuwa umeshafanywa na wasanii wengi, mimi nikaongezea wa kujipaka mafuta mengi na wanja ubunifu ambao sikuwahi kuuona kwa msanii yeyote," amesema Ebitoke.

Amesema iwapo ataibuka msanii na kujipaka mafuta mengi katika vichekesho, basi atakuwa amemuiga yeye (Ebitoke), ambaye anajinasibu kuwa ni mwanzilishi wake.



BODA 2 BODA

# Tony Boy kuanzia Nairobi

MKONGWE wa muziki wa kizazi kipya, Matonya, amejichimbia jijini Nairobi Kenya kwa ajili ya kushuti video ya wimbo wake wa 'Tonya Boy', ambao ni wa kwanza kwa mwaka huu.

Ameiambia BT kuwa ameamua kwenda jijini humo ili kupata mandhari tofauti, kwa vile video zake nyingi amekuwa akishuti hapa nchini.

"Unajua kwa sasa soko la muziki ni kama limebana sana, hivyo nimeona niangalie uwezekano wa kuibuka na wimbo mpya ukiwa na video ilioandaliwa nje ya nchi," amesema Matonya.



## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Kuwa** makini na wanaoeleza matatizo yako kwa watu wakijifanya kukuonea huruma au kusikitishwa na hali yako. Wengi wao wanataka tu matatizo yako yajulikane. Lengo lao ni kukusambazia na siyo kukusaidia. Usiwaeleze zaidi ya wanachotakiwa kujua - **Nikki wa Pilli.**



**Mungu** anaweza kukunyima ndizi moja asubuhi, halafu akakupa mkungu mzima wa ndizi jioni. Kikubwa ni kuwa na subira tu - **Johari.**




**Umeyakuta** kwa nini yakutese? - **Aunt Ezekiel.**

# Kuumbe!

## Chege hii inshu ya Mbosso ni kweli?





**Na Adam Fungamwango**

MSANII Chege amefunguka na kusema kuwa hana chuki na mtu yoyote yule tofauti na watu wanavyodai.

Chege, mmoja wa waasisi wa TMK Wanaume anasema hayo kufuatia madai kwamba alimshawishi msanii Mbosso kutojiunga na WCB.

Ikumbukwe kuwa awali Mbosso alikuwa kwenye kundi la waliokuwa vijana wadogo wakati huo la Yamoto Band.

Akiulizwa kuhusu madai hayo, Chege alisema kwanza hajasikia chochote kuhusu madai hayo, lakini pia hajawahi kumshauri mtu kitu kama hicho na pia hana chuki na mtu yoyote, achilia mbali msanii.

"Sijawahi kuwa na chuki na mtu, kwa hiyo siwezi kuliongelea hilo kwa sababu nitakuwa muongo." anasema na kuongeza.

"Kwanza sijasikia chochote kama kuna watu au mtu ameongea nini na nikishasikia, ndiyo naweza kujibu au kuongea, " anasema.


Pamoja na mengineyo, Chege aliongea hayo akiwa kwenye maandalizi ya kutoa ngoma yake mpya iitwayo 'Manjegeka', akimshirikisha msanii wa kike, Venessa.

"Tumemaliza kufanya 'shooting' na muda wowote kuanzia sasa tunaweza kuiachia, mwaka huu nataka kutoa vitu vichache, lakini vyenye nguvu," anaongeza msanii huyo.

Majuzi, msanii mmoja mkubwa nchini alidai kwamba Chege alikuwa mmoja wa watu waliokuwa wakimshawishi Mbosso kutojiunga na WCB, lakini kwa sasa amekuwa na mafanikio makubwa kiasi cha kupiga shoo za maana akiwa kwenye lebo hiyo, akilipwa kiasi kikubwa cha pesa hadi milioni 30,000 kwa shoo moja.



# WANAMUZIKI WA 5 WAGENI WENYE SAUTI TAMU



**Na Adam Fungamwango**

KWENYE safu hii tulishawahi kuwaweka wanamuziki wanaoimba sauti ya kwanza, lakini wote ni Watanzania.

Tuliwapata kina Eddy Sheggy, Nasri Lubua, Hassan Bitchuka na wengineo.

Leo hii tutawaangalia wanamuziki wanaoimba sauti ya kwanza, lakini hawakuwa Watanzania.

Nchi hii ilibahatika kupata wanamuziki bora, wenye viwango vya hali ya juu kutoka nje ya nchi na kuja kuchuana na Wabongo.

Wanamuziki hawa walikuja na kujiunga na bendi mbalimbali nchini, wengine wakija na bendi zao kutoka walikokuwa.

Baadhi ya wanamuziki hao walikuwa waimbaji wa sauti ya kwanza na ya juu ambao walijipatia umaarufu mkubwa na kuwa mastaa kiasi kwamba hata leo bado wanaendelea kukumbukwa kwa kazi kubwa walioifanya.

**MBUYA MAKONGA 'ADIOS'**

Ni mwimbaji wa sauti ya kwanza kwenye bendi ya Maquiz Du Zaire na baadaye ilijulikana kama Maquiz Original.

Adios alikuwa mmoja wa viongozi na waanzilishi wa bendi hiyo iliyoingia nchini mwanzoni mwa miaka ya '70 ikitokea nchini Zaire wakati huo sasa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo.

Nyimbo nyingi za bendi hiyo maarufu kama 'Dora Mtoto wa Dodoma', 'Mokili', 'Nimepigwa Ngwala', 'Kasongo', na nyingine nyingi zote ameimba sauti ya kwanza. Alifariki dunia mwanzoni mwa mwaka 2000 na kuacha alama kwenye tasnia ya muziki wa Tanzania.

**KABEYA BADU**

Huyu anajulikana zaidi kama mwimbaji wa bendi ya Orchestra Safari Sound (OSS) ikiwa na mtindo wa Masantula na Dukuduku.

Lakini awali aliingia nchini akitokea Kongo na kujiunga na bendi ya Maquiz miaka ya mwishoni mwa miaka ya '70. Lakini kutokana na kukuta magwiji, hasa Mbuya Makonga, hakupata namba sana na jina, hivyo alitimkia OSS mwanzoni mwa miaka ya '80 na kuwa mwimbaji wa sauti ya kwanza kwenye nyimbo nyingi za bendi hiyo.

Huyo alipata umaarufu mkubwa kwa kuimba na kutunga nyimbo nyingi. Mfano wa wimbo uliompa umaarufu ni 'Ziada'.

Alifariki dunia 2013 akiwa kwenye bendi ya Ya Capital 'Wazee Sugu'.

**BAZIANO BWETI**

Wale wakongwe wanamkumbuka tangu mwanzoni na katikati ya miaka ya '60 hadi '70 akiwa na bendi maarufu wakati huo, Orchestra Fauvette akiwa na kina Ndala Kasheba na King Kiki wakati bendi hiyo ilipozuru nchini ikitokea Zaire. Bendi hiyo baadaye ilijukana kama Safari Nkoy. Baadaye hakusikika baada ya kurejea kwao, huku wenzake kina Kiki na Ndala wakitamba na bendi mbalimbali nchini. Alirejea nchini mwishoni mwa miaka ya '80 na kujiunga na Zaita Musica akiimba sauti ya kwanza hadi alipofariki dunia mwanzoni mwa mwaka 2000.

**NICO ZENGEKALA**

Tanzania ilipata bahati ya kuwa na mwimbaji mwenye sauti tamu mithili ya maji ya yanayotiririka kwenye maporomoko. Huyu anaitwa Nicolaus Zengekala. Mwimbaji huyo mlemavu wa macho alikuwa ni raia wa Kenya sehemu za Mombasa. Aliingia nchini miaka ya '80 na baadhi ya wanamuziki wa Mbaraka Mwinshehe walioamua kurejea nchini kutoka Kenya baada ya kifo cha mwanamuziki huyo mwaka 1979. Wanamuziki hao wakiwa na Nico, wakiwa Morogoro waliifufua bendi ya Les Cuban Marimba na nyimbo za 'Jackie', 'Shemango', zilizoimbwa na Zengekala ziliwapatia umaarufu mkubwa.

Juwata Jazz ilimnyakua mwanamuziki huyo na kuzidi kumfanya kuwa staa mkubwa nchini na Msondo, kuzidi kuwika.

Nyimbo kama 'Solemba', 'Bahati', Hasira Hasara', 'Prisila', 'Mahmoud' akiimba kwa ustadi mkubwa zilizidi kumfanya kuwa na mashabiki wengi nchini. Alifariki dunia Desemba 17, 1987 jijini Dar es Salaam na kuzikwa kwao sehemu za Mwatate, Mombasa nchini Kenya wiki moja baadaye.


**LOVY LONGOMBA**

Aliingia nchini akitokea Kenya alikowika akiwa bendi kubwa kabisa nchini Kenya ya Super Mazembe akiwa ameimba na kutunga nyimbo nyingi kama 'Ouma', 'Atia', 'Gina', 'Loboko', 'Mado Zaina' na nyingine. Pamoja na kutokea Kenya, lakini alikuwa ni Mkongomani. Alikuwa na sauti kali na ya juu mithili ya kike, kitu ambacho kiliwachanganya wengi wasijue anayeimba ni mwanamume au la. Hata wanamuziki wa Afriso Ngoma hawakuamini bosi wao alipowaambia kuwa atawaletea mwamuziki mkubwa Afrika Mashariki. Lovy, aliiletwa nchini na Juma Mwendapole aliyekuwa mmiliki wa bendi hiyo. Akiwa Afriso alitunga nyimbo kama 'Ule Baba Watoto', 'Salima', 'Kaebego', 'Linda', Imbe' na nyingine nyingi.

Alifariki dunia mwaka 1996 kwa ajali ya gari eneo la Kambi ya Chokaa huko Arusha wakati basi la abiria la Taqrim alilokuwa amepanda kugonga lori kwa nyuma akiwa mmoja wa abiria watano waliofariki.

# Vijimambo

PICHA ILIYOPITA



1. Matokeo ya 'punguzo la bei' ndio hayo sasa - Mama Nah, Manzese DSM.
2. Walisema wahenga, pombe siyo chai. Unaona sasa mlinzi kalala - Mama Nah, Manzese DSM.
3. Hili joto likiendelea navua mpaka ngozi yangu - Beneali Moussa Beneali, Migombeni Zenji.
4. Si utani, babake alipania sana punguzo la bei la Kwa Mkapa - Elisante Mbunda, Manyoni Singida.
5. Daaah! Huyo lazima atakuwa 'afande' wa walinzi halafu kalewa - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
6. Mambo hayo fanya huko huko Dar, Iringa unapotelea kwenye sufuria - Deo Sanga, Makete Njombe.
7. Babu vipi, viatu vimekuchosha nini? - Adinani Mrutu, Kiwalani DSM.
8. Tatizo la kilevi bila kula nyama - Shirima, Morogoro.
9. Ni pozi tu jamani, wala msinijaribu - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
10. Kwa hili joto la mjini, ngoja nijinafasi kwenye kaupepo - Agatha Mbale, Moro Town.
11. Mbwa huko kijijini, mjini wote watu - Michael Mbatta, Makumbusho DSM.
12. Acha kukoroma na ulevi wako wewe, bisi wako anakuja utafukuzwa kazi - Annah Gumbo, DSM.
13. Mmenilisha biskuti mnashangaa nini nikivaa kama nyinyi? - Michael Mbatta, Makumbusho DSM.
14. Ama kweli mbwa wa mjini wanafaidi, wanavaa mpaka milegezo! - Athanas Gumbo, Mbagala DSM.
15. Leo nimetinga suruali, kesho namalizia koti na tai - Flora, Temeke.
16. Unapoingia Sumbawanga usiwe mjuaji saaana, yatakukuta kama huyu jamaa - Mfaume Mbugi, Mshindo Iringa.
17. Ngoja wezi wanione mlevi, halafu watajua kwa nini nilifanywa kuwa mlinzi - Baby Natasha, Magomeni DSM.
18. Jamani sijalewa, nasumbuliwa na malaria kali - Butelezi Bunyoro, Mwandiga Kigoma.
19. Hapa sasa kausingizi katakuja, koti lilikuwa na joto balaa! - Simon Mvungi, Sinza DSM.
20. Ushauri wa bure. Siku nyingine usifakamie pombe za bure - Mama D., Michenzani Zenji.
21. Naona kibarua chake kinaota nyasi hivi hivi. Sio kwa kulewa na kulala huko - Mahija Jumbe, Ngamiani Tanga.
22. Sio siri, pombe za leo zilikuwa tamu sana tatizo hazikuwa na asusa. Ona nilivyolewa - Mahija Jumbe, Tanga.
23. Ulinzi umenishinda, niache nilale - 0654 865 436.
24. Kwa hili baridi la Iringa, bora nilale kwa kuvae suruali na viatu - Abousalim, Singida.
25. Ulivamia vitumbua ukidhani nyama eeeh! Ona vilivyokulewesha sasa - Mariam Beneali, Migombani Zenji.

**SMS Bomba ya Leo:**
***Jamani sijalewa, nasumbuliwa na malaria kali - Butelezi Bunyoro, Mwandiga Kigoma.***

PICHA MPYA



**TUMA MESEJI - 0773 477 311**



# Msamaha wa Rais binadamu hupanga, Mungu hupangua

**Na Adam Fungamwango**

BINADAMU hapa duniani wana tabia ya kupanga mipango yao mbalimbali ya maisha ya kila siku.

Hata hivyo, hufanikiwa kama tu Mwenyezi Mungu anapenda. Vinginevyo hakuna kitu ambacho Mungu anakataa kisifanyike kwa binadamu kikafanikiwa.

Filamu ya 'Msamaha wa Rais' unaonyesha ni jinsi gani binadamu anavyoweza kupanga, lakini kumbe Mungu amepanga vingine kabisa.

Imechezwa na wasanii ambao si maarufu sana, lakini wenye uwezo mkubwa. Inaanza kwa mama Ndimbo akiwa anafagia uwanja asubuhi.

Kwa mbali anaona mtu kama mtoto wake Mapunda aliyehukumiwa kwenda jela miaka 30 kwa kosa la mauaji. Anaona kama ndoto, kwani ni miaka mitatu imepita tangu ahukumiwe.

Anapofika karibu anagundua kuwa ni kweli alikuwa Mapunda, anamkumbatia na kumfanyia mila, kabla ya kuingia ndani. Mdogo wake Mapunda aitwaye Ndimbo anaporejea matembezini na kuambiwa kuwa kaka yake amerejea uraiani, anashtuka na kusononeka badala ya kufurahi. Anamuuliza mama yake kwa nini amerejea uraiani mapema wakati alihukumiwa miaka 30.

Mama anamjibu kuwa ameachisa kwa msamaha wa Rais. Kuna kitu kimefanyika miongoni mwao, wakidhani kuwa Mapunda atazeekea jela miaka 30, miaka ambayo asingerejea leo wala kesho, lakini mipango yote imevurugika.

Wakati wakiteta hayo, Mapunda hakuwapo kwani alishaanza kuzunguka mitaani. Anakwenda kumuona mchumba wake Anna nyumbani kwao.

Hata hivyo, hakukutana naye. Cha ajabu inaonekana kama vile kuna jambo ambalo linafichwa juu yake, kwani kila anapokwenda kwa mchumba wake hamkuti, mchumba mwenyewe hamtafuti mwenzake aliyerejea, lakini hata nyumbani kwao kuna wakati anamkuta mama yake na mdogo wake Ndimbo kuna kitu wanateta.

Anabaini kuwa mchumba wake Anna ni mjamzito baada ya kumfuma laivu. Ni ujauzito wa nani wakati yeye alikuwa jela? Mtihani mwingine. Inakuwa ni siri ya kijiji.

Hakuna yoyote kijijini hapo anayetoa siri, licha ya kwamba anajua kila kitu. Anna mwenyewe pamoja na kupigwa na mchumba wake, lakini hajathubutu kusema.

Anakutana na dada mmoja na kumtishia kumuua. Kutokana na vitisho anaamua kumwambia kuwa mimba ya Anna ni ya mdogo wake Ndimbo. Anarejea na kukutana na mdogo wake, anaanza kumpiga.

Ni kipigo kitakatifu, Anna anafika na anapotaka kuamulia, anasukumwa na Mapunda mpaka chini. Uchungu wa kujifungua unamshika. Mapunda na mdogo wake Ndimbo wanaacha kupigana ili kumsadia Anna. Kuna mama anapita na wanamuomba awasaidie. Anna anajifungua. Mapunda anaamua kumuachia ndugu yake Ndimbo mwanamke na yeye anaamua kuondoka kijijini kwenda sehemu nyingine kutafuta maisha.

# ABETI MASIKINI

## Aliyewasuka Mbilia Bel, Yondo Sister, Tshala Muana



ELISABETH Jean Finant au maarufu kama Abeti Masikini, ni mwanamuziki maarufu wa iliyokuwa Zaire, sasa Jamhuri ya Kidemokrasi Congo (DRC).

Abeti alizaliwa Novemba 9, mwaka 1954 mkoani Kisangani katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na alifariki Septemba 28, 1994 huko jijini Paris, Ufaransa.

Miaka zaidi ya 24 sasa hayupo duniani, bado anakumbukwa kwa kusakata na kupiga muziki na alitambulika sana.

Jina la Abeti Maskini, ndilo lililotawala, huku akiwa umarufu wa kuimba kwa Kiswahili, wimbo uliotamba ni 'Likayabu' au 'Manjano na Amdalasini.'

Kimaumbile, Abeti alikuwa 'chotara' baba yake mzazi ni mchanganyiko wa Mkongomani na Mbelgiji na mama, mkongomani halisi.

Muziki na maisha

Abeti alikuwa fundi wa muziki, tangu zama za umri mdogo akiwa katika umri mdogo sana, ambao hakuna aliyetegemea hasa kwa jinsia yake.

Mbali na hapo, pia ana historia ya mafanikio, kwamba aliwawezesha baadhi ya wanamuziki waliokuja kuwa kioo cha kimataifa, kwa historia ndefu ya kuwasuka hasa.

Hao ni Mbilia Bel na Tshala Muana. Mbilia Bel alikaa katika chungu cha Abeti na kupikwa vilivyo kuanzia kuimba hadi kunengua kuanzia mwaka 1976 hadi 1981.

Naye, Tshala Muana alianza mwaka 1978 hadi 1979, huku akitajwa mwanamuziki maarufu,Yondo Sister, naye alipikwa na Abeti mwaka 1986.

Mwingine ni mwanamama Abby Surya, aliyemsuka muziki kati ya mwaka 1984 hadi 1986.

Kwa upande wa wanaume, waliofanya kazi na kuinuliwa na mwanamama huyo, ni pamoja na Malage De Lugendo, Lokua Kanza na Komba Bellow. Ujuzi wa muziki wake uliwafanya wanamuziki wengine wa muziki mtindo wa 'Sokous' na 'Aurlus Mabele' kupenda kazi za Abeti kupita kiasi.

Sifa aliyowaathiri Mbilia Bel na Tshala Muana ni kupenda kutunga au kuimba nyimbo zao kwa lugha ya Kiswahili.

Mfano hai ni wimbo wake wa Likayabu (Manjano na amdalasini), na hata albamu yake ya 'Kupepesuka' ya mwaka 1978.

Historia ya kifamilia, ni kwamba baba yake, Mzee Jean Finant, aliuawa mwaka 1961 mjini Mbuji Mayi, kutokana na matatizo ya kisiasa na mama yake alilazimika kuhama nao hadi jijini Kinshasa, alikosoma na kuhitimu sekondari.

Baadaye aliajiriwa katika Ofisi ya Waziri wa Utamaduni wakati huo. Kwa upenzi wa muziki, ilimlazimu aache kazi na kuendelea na muziki.

Ilikuwa mwaka wa 1971, yaliandaliwa mashindano ya kutafuta mwanamuziki chipukizi na yeye akamuua kujitosa. Alilazimika kuacha kazi, ili pasionekane upendeleo kwa mtumishi wa wizara husika. Alipata nafasi ya tatu, ambayo ndio chimbuko lake rasmi katika muziki.



# Alicios avutiwa na muziki wa Bongo

KIMWANA Alicios Theluji kutoka nchini Kenya, amekiri kwamba wasanii wa Tanzania wanajituma zaidi na anaona wa kike pia wamo.

"Kuna kolabo nzuri kati ya wasanii na pia vyombo vya habari vya Tanzania na vinasaidia kuufikisha muziki mbali zaidi na muziki unakuwa mkubwa," amesema Alicios.

Amesema kwa upande wake huwa hashindani na mtu kwa kuwa muziki ni hisia na hatafuti kuandika na kufanya kile ambacho anahisi, hivyo kama hakipendwi, kwake ni sawa tu.



## Mwenye nyumba amburuza Blac Chyna

BLAC Chyna anadaiwa dola za kimarekani 48,000, ambazo ni sawa na zaidi ya Sh. milioni 100 za Kitanzania ikiwa ni kodi ya nyumba aliyopanga.

Mtandao wa The Blast umeripoti kuwa Chyna amefunguliwa mashtaka na mwenye nyumba wake baada ya kushindwa kulipa kodi hiyo.

Baba mwenye nyumba wake, Michael Kremerman, amefungua mashtaka na kudai mwaka 2017 Blac Chyna aliingia mkataba wa kuishi mwaka mmoja katika nyumba ya vyumba sita, mabafu matano na studio na kwamba gharama yake ilikuwa ni dola za kimarekani 16,000 sawa na zaidi ya Sh. milioni 37 za Kitanzania ikiwa ni kodi ya mwezi.

Michael Kremerman alidai kuwa Chyna aliongeza mkataba hadi Machi 31, 2019, lakini Novemba 2018 alihama, ambapo miezi iliyobaki ili kumaliza mkataba hakuwa analipa kodi.

## Hili ndilo shavu jipya la rapa DMX

RAPA DMX amepata shavu ikiwa ni miezi michache imepita tangu amalize kifungo chake. DMX anatajwa kurejea kwenye filamu yake ya kwanza iitwayo 'Chronicle Of A Serial Killer' iliyopo chini ya muongozaji Steve Stanulis.

Kwa mujibu wa mtandao wa Hot New Hip Hop umeripoti kuwa rapper huyo ndio muigizaji mkuu, ambapo uhusika aliopewa ndani ya filamu hiyo ni kuwa kiongozi wa upelelezi na kwamba utengenezaji utaanza June mwaka huu jijini New York.

"Sina mashaka na DMX ataleta kitu cha tofauti kwenye nafasi yake ya uigizaji, nina furaha kuwa miongoni mwa waigizaji wenye vipaji katika hii filamu, nina matumaini ya kufanya naye kazi na watu wengine kwenye kipindi hiki," amesema Steve Stanulis.





## Nyumba ya Chris Brown kukaguliwa

MTANDAO The Blast umeripoti kuwa, msanii Chris Brown, amemruhusu mwanamke anayetajwa kwa jina la Jane Doe, kufanya ukaguzi katika nyumba yake mjini Los Angeles baada ya mwanamke huyo kumfungulia mashtaka ya ubakaji miezi kadhaa iliyopita.

Kwa mujibu wa nyaraka za mahakama, ni kwamba zitamruhusu Jane Doe kufanya ukaguzi katika nyumba hiyo akisindikizwa na mawakili wawili na mpiga picha ili kufanya uchunguzi katika vyumba vyote vya msanii huyo.

Aidha, Jane Doe ataruhusiwa kurekodi tukio zima bila video hizo kuwa na sautin na huenda akakumbuka mazingira aliyekuwepo wakati anafanyiwa tukio hilo.


## Justin Bieber ang'ang'aniwa mahakamani

MPIGA picha William Wilson, amemshtaki msanii Justin Bieber baada ya msanii huyo kumgonga kwa gari wakati akitoka kanisani jijini Los Angeles.

Hii ni kwa mujibu wa mtandao wa TMZ, William Wilson amedai mbele ya mahakama kuwa ni uzembe uliosababisha ajali hiyo iliyotokea mwaka 2017 na kusema alikuwa amesimama upande wa waenda kwa miguu na ndipo Justin Bieber alipolipeleka gari na kumgonga.

Kwa upande wake Justin Bieber alijitetea na kusema waandishi walishuhudia tukio hilo na hakufanya makusudi bali ajali hiyo ilitokea kutokana na matatizo ya kiafya.

Inaelezwa kuwa Justin Bieber alionyesha ushirikiano kufuatia gari la wagonjwa kufika na kumchukua William, huku taarifa za polisi wa Beverly Hills zikisema kuwa Justin Bieber alishirikiana nao vyema hivyo hakufunguliwa mashtaka.



SAFU



Mionzi ya Sheria

# Tuuenzi Muungano wetu, wajibu wa kuulinda kisheria huu hapa

Na John Juma
0716217615

JANA ilikuwa siku ya mapumziko kitaifa, kuadhimisha Miaka 55 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, tangu kuasisiwa kwake, Aprili 26 mwaka1964.

Huo ni wajibu uliotokana na ukweli kwamba, Taifa letu ni tunda au zao la kuungana kwa nchi mbili huru.

Kuna ule usemi wa Kiswahili: "Umoja ni nguvu na Utengano ni udhaifu." Huo ni mtazamo au fikra ambayo alikuwa nayo hayati Sheikh Abeid Amani Karume, mapema sana mara baada ya kufanikiwa.

Anaieleza katika kauli: "Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar", ilyofikia ndoto yake: "Muungano wa Jamhuri ya Tanganyika na ile ya Watu wa Zanzibar."

Ukweli huo unathibitishwa na kauli ya Hassan Juma Khamis (82), aliyekuwa dereva binafsi wa Mzee Karume, kabla hajawa Rais wa Zanzibar na hatimaye baada ya uhuru kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu.

Kinachoitwa 'Mkataba wa Muungano' ulitiwa saini na Mwalimu Julius Nyerere na Abeid Amani Karume, Aprili 22, mwaka 1964, huko Zanzibar.

Ni mkataba uliothibitishwa na Bunge la Tanganyika pamoja na Baraza la Mapinduzi, Aprili 26 na 27, mwaka 1964. Viongozi hao walikutana katika ukumbi maarufu wa Karimjee, jijini Dar es Dalaam kubadilishana hati (hizo) za Muungano.

Sheria za Muungano zinapambanua (kwa wakati huo), Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar zililazimika kuwa dola ya Jamhuri kwa jina la "Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar."

Jina hilo la 'Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar' lilibadilishwa baadaye kidogo, tarehe 28 Oktoba, 1964 na kuwa 'Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.' kupitia Sheria ya Jamhuri ya Muungano, Namba 61, ya mwaka 1964.

Hivyo basi, msingi mkuu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na hata ile ya Zanzibar, 1984, ni Hati za Muungano za Mwaka 1964, ambazo zilitiwa saini na Mwalimu Nyerere na Sheikh Karume, Aprili 22, 1964 na kisha Tanganyika na Zanzibar kuwa dola moja kwa misingi inayotambulika kimataifa.

Baada ya kuundwa Muungano, Mwalimu Nyerere akawa Rais wa kwanza na Mzee Karume Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kimsingi, mara baada ya hatua ya Aprili 26, 1964 Bunge la Tanganyika kupitisha Sheria za Muungano na kufuatiwa na uthibitisho kutoka kwa Baraza la Mapinduzi Zanzibar siku iliyofuatia, Aprili 27 ya mwaka huo huo, wajumbe saba wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, waliapishwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Hao Amani Abeid Karume, Kassim Abdallah Hanga, Abdurrahman Babu, Hassan Nassor Moyo, Aboud Jumbe, Hasnu Makame na Idrisa Abdul Wakil. Hiyo ilikuwa baada ya waasisi kubadilishana Hati za Muungano.

**WAJIBU KIKATIBA**

Ibara ya 46B (1) inaelekeza kama ifuatavyo: "Bila ya kuathiri wajibu wa kila raia uliotajwa katika Ibara ya 28 ya Katiba, viongozi wakuu wa vyombo vyenye mamlaka ya utendaji katika Jamhuri ya Muungano vilivyotajwa katika, Ubara ya 4 ya Katiba, watawajibika kila mmoja wao katika kutekeleza madaraka aliyopewa kwa mujibu wa Katiba au Katiba ya Zanzibar 1984, kuhakikisha kuwa analinda, kuimarisha na kudumisha umoja wa Jamhuri ya Muungano.

Ibara Ndogo ya Pili; inaendeleza mkazo katika madhumuni ya masharti ya ibara ndogo ya kwanza, kila mmojawapo wa viongozi wakuu wa vyombo vyenye mamlaka ya utendaji katika Jamhuri ya Muungano, kabla ya kushika madaraka yake kwa mujibu wa katiba, ataapa kuitetea na kudumisha umoja wa Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa katiba iliyopo.

Ibara Ndogo ya Tatu; viongozi wakuu wanaohusika na masharti ya ibara husika, ni Rais wa Jamhuri ya Muungano; Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano; Rais wa Zanzibar na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano.

Pia, Ibara ya 28 (1) nayo imeweka wajibu: Kila raia kulinda, kuhifadhi na kudumisha uhuru, mamlaka, ardhi na umoja wa taifa.

Jambo hilo, kwa lugha au maana iliyojificha, linakusudia wajibu wa kulinda na kutunza Muungano uliopo.

Naam! Hiyo ndiyo hadithi fupi kuhusu Muungano uliowezesha kuzaliwa tunda ya mtoto aitwaye Tanzania, sambamba na jukumu la viongozi wa kitaifa kuhakikisha unaendelea kuwapo kwa maslahi mapana ya pande zote mbili.

Mwito muhimu, ni kwamba: "Tulinde na Kuudumisha Muungano wetu; kuijenga Tanzania yetu (bila ya wenyewe hakuna Watanzania) kwa fahari ya Waasisi wa Uzalendo wetu."



Kalamu ya Mwalimu

# Kambi za kitaaluma zinavyowapa wanafunzi muda unaotosha kusoma

Reubeni Lumbagala

MWANAFUNZI anapaswa kutenga muda wa kutosha kujisomea, ili yale anayofundishwa darasani na walimu wake, yaendelee kukaa katika ubongo wake, hatimaye aweze kufaulu vizuri masomoni.

Bila ya kujisomea, hakuna kufaulu kwa mwananfunzi. Ndiyo maana, wanafunzi wanashauriwa kuwa na ratiba zao binafsi za kujisomea, mbali na ratiba za vipindi vya darasani zilizopo shuleni.

Zipo changamoto kwa wanafunzi wengi, hasa shule za msingi na sekondari za kutwa, kushindwa kujisomea ipasavyo, kutokana na uhuru mkubwa walio nao, pindi wanaporejea majukwaani kwao baada ya vipindi vya shule.

Changamoto hiyo inachangia kushuka ufaulu wa wanafunzi wanaosoma katika shule za kutwa na ndiyo maana juhudi mbalimbali zimekuwa zikifanywa na serikali, kwa kushirikiana na sekta binafsi, asasi za kiraia, wadau wa elimu na wananchi kwa ujumla kuhamasisha ujenzi wa mabweni katika shule za msingi na sekondari.

Kwa kuwa gharama ni kubwa katika kutekeleza azma hiyo ya ujenzi wa mabweni, serikali inalitekeleza hilo kwa awamu, baada ya awamu kulingana na upatikanaji fedha huku juhudi za kuhakikisha wanafunzi wanapata muda wa kutosha wa kujisomea zikiendelea kufanyika.

Njia mojawapo inayotumiwa na serikali ni kupitia uongozi wa ofisi za elimu za mikoa na wilaya, kwai kuanzisha kambi za kitaaluma, ili kuwapa wanafunzi muda wa kutosha wa kujisomea.

Hiyo inafanyika hasa kwa wanafunzi wanaosoma katika madarasa yenye mitihani ya Taifa, kama vile darasa la nne na la saba, pia vidato vya pili, nne na sita.

Kambi za kitaaluma ni hali ya wanafunzi kukaa shuleni muda wote, kama ambavyo wanafunzi wa bweni wanavyoishi. Katika kambi hizo, wanafunzi huishi kwa kufuata na kuzingatia taratibu zote zinazoongoza shule za bweni.

Wazazi na walezi hushiriki kwa kuchangia chakula kitakachotumika kulisha watoto wao na kuwapatia mahitaji muhimu, kama vile mafuta ya kujipaka, sabuni na fedha kidogo za kujikimu.

Hivyo, kambi za kitaaluma huwaandaa wanafunzi kuanza kuzoea maisha ya bweni na hii huwasaidia kuendana na mazingira ya bweni pindi wanapojiunga na shule za bweni baadae.

Wanafunzi wanaokaa katika kambi hizo, hupata muda wa kutosha kujisomea hasa muda wa jioni na usiku, kwani mazingira ya kambi huwalazimu kujisomea.

Kutokana na wanafunzi kukosa muda wa kuzurura mitaani na usimamizi thabiti wa walimu katika kambi za kitaaluma, wanafunzi hulazimika kujisomea zaidi.

Ni hali inayowasaidia kujifunza vitu vingi na hatimaye kufikia malengo yao ya kufaulu mitihani. Mwanafunzi awapo kambini, haruhusiwi kulala bwenini wakati wenzake wakijisomea, kama hana sababu ya msingi kama vile kuumwa.

Ni rahisi kwa mwanafunzi awapo katika mazingira ya nyumbani kwao, akalala bila ya kujisomea na hata kama hana sababu ya msingi inayomzuia kusoma.

Kambi za kitaaluma, pia zinatoa uhuru kwa wanafunzi kujisomea muda wowote na kwa utulivu mkubwa. Licha ya wanafunzi kuwekewa ratiba ya kujisomea nyakati za usiku, lakini bado mwanafunzi ana uhuru wa kuendelea kujisomea kwa kadri ya uwezo wake pindi muda wa wanafunzi wote kujisomea unapokwisha.

Mwanafunzi anao uhuru wa kulala na kuamka usiku kuendelea kujisomea apendavyo, kabla ya kuanza siku mpya ya masomo.

Katika mazingira hayo, mwanafunzi anajikuta anasoma katika hali ya utulivu mkubwa na kuingiza maarifa mengi kupitia madaftari na vitabu anavyojirejea. Ni mazingira adimu sana kupatikana katika nyumba nyingi, kwa wanafunzi wanaosoma shule za kutwa. Faida nyingine ya kambi za kitaaluma ni kumsaidia mwanafunzi kuchangamana na wenzake wakati wa kujisomea. Ni muhimu kwa mwanafunzi kusoma na wenzake, ili kushirikishana uelewa katika mada mbalimbali za masomo yao.

Wakati mwingine kutokana na umbali baina ya makazi ya wanafunzi, inakuwa ngumu kwao kusoma kwa pamoja. Kupitia kambi za kitaaluma, wanafunzi wanachangamana kujifunza pamoja.

Ipo wazi kwamba, uelewa wa wanafunzi unatofautiana kati ya mmoja na mwingine. Wanaposoma pamoja ni njia mojawapo ya kusaidiana wenyewe.

Hamisi Kipita, ni Mwalimu wa Shule ya Msingi Chimehe, mkoani Dodoma. Anashauri shule nyingi zianzishe utaratibu wa kuwaweka wanafunzi kambini, ili kuwapa muda wa kutosha wa kujisomea.

Kipita anasema:"Kambi ni nyenzo muhimu ya kuongeza ufaulu katika shule za msingi na sekondari. Sehemu mbalimbali ambazo zimefanya makambi ya kitaaluma kama Simiyu, Njombe na Dodoma, zimeonyesha mabadiliko chanya katika ufaulu wa wanafunzi wao, upo umuhimu wa kambi hizi kuwekewa mkazo katika Halmashauri zote nchini."

Wanafunzi walioko kambini, wahakikishe wanatumia fursa hiyo kujisomea kikamilifu, ili waweze kufaulu vyema katika mitihani yao na kujenga mustakabali mwema wa maisha yao kupitia elimu.

**●Reubeni Lumbagala ni Mwalimu kwa Taaluma kutoka Shule ya Sekondari Mlali iliyopo wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.**
**Kwa maoni piga simu: (+255) 0764 666349.**

# MASIKINI MARIAM...

# Kidonda sugu kil waziri wake wan

**Na Romana Mallya**

■Alijieleza mtandaoni alivyo maskini
■Daktari bingwa, dada waanika ilivyo
■Sasa kila kitu serikali imechukua 100%

NI Wiki hii tiba yake imehamishiwa rasmi katika Taasisi ya Saratani Ocean Road, jijini Dar es Salaam, akiwa mikononi mwa matabibu wanaompigania .

Lakini ikirejewa, ni safari ya maisha iliyoambatana na maumivu makali kwa msichana Mariam Rajab (25), ambaye kwa miaka mitano sasa, amekuwa akitibu kidonda sugu kilichopo mgongoni mwake.

Mariam, ni mtoto wa nne kati ya watano waliozaliwa na Mzee Rajab, mkazi wa Kitongoji cha Inung'una mkoani Singida, anayekiri mateso makali na maumivu yaliyopitiliza, huku umaskini ukitawala familia yake kushindwa za kugharamia Sh. 5,000 kila siku, kusafishwa kidonda hicho hospitalini.

Mariam ambaye kwa muonekano ni msichana mrembo, lakini maumivu anayopitia, yamemuondolea furaha usoni mwake.

Ni wiki moja na nusu sasa, alipelekwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), baada ya kurushwa video fupi mitandaoni akiomba msaada wa matibabu kwa wasamaria, kutokana na umaskini wa familia yake inayoshindwa kumudu gharama za matibabu.

Katika video hiyo fupi, Mariam alisikika akilalama: "Naishi familia ya kimaskini, wazazi wangu hawana uwezo wa kunisaidia tatizo langu ambalo ninalo ambacho ni kidonda kilichopo mgongoni."

**SAFARI YA MUHIMBILI**

Baada ya hapo, Mariam alikionyesha kidonda chake. Ni ujumbe uliopokewa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliagiza Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kumtafuta na kuhakikisha anafikishwa hapo kuanza matibabu.

Usiku wa kuamkia Alhamisi ya tarehe 18 mwezi huu, Mariam akiwa kwenye gari maalum la wagonjwa (ambulance), alifikishwa hospitalini Muhimbili, akitokea kwao Singida.

Hadi siku chache zilizopita, tayari alikuwa amelazwa katika Wodi Namba 15, iliyopo jengo la Kibasila na tayari Daktari Bingwa Mkuu wa Idara ya upasuaji hospitalini hapo, Ibrahim Mkoma, alishamfanyia vipimo, siri ya usugu wa kidonda hicho.

Mariamu akiwa katika maumivu hayo makali, anasimulia mateso yake yenye miaka mitano sasa.

**ASIMULIA MKASA**

Mariam anaanza kusimulia anavyoteseka na kidonda hicho ambacho chanzo chake kuungua moto. Anasema, alitibiwa katika Hospitali ya Mkoa Singida, hadi kilipoonekana kimepona.

Anasema baada ya kupona kovu la moto eneo hilo la mgongo lilitokea jipu, ambalo baadaye lilipasuka. Anaendelea: "Lilipopasuka nikawa naenda hospitalini kusafishwa, lakini kadri siku zilivyoendelea kidonda kiliongezeka."

"Gharama za kusafishwa kila siku zilikuwa Sh. 5,000. Kama nilivyoeleza, familia yetu ni maskini hivyo haikuweza kuzimudu," anasema.

Mariam anasimulia kwamba, aliendelea na huduma ya kusafishwa kila siku hospitalini na kuanzia mwezi Agosti mwaka jana, ilibidi awe anapewa huduma hiyo na ndugu zake nyumbani, kutokana na uhalisia wa ugumu wa maisha yao.

"Kadri kilivyokuwa kinasafishwa nyumbani, kidonda kikawa kinaendelea kukuwa na mwisho wa siku kikafikia ukubwa huu. Wakati nasafishwa nyumbani, kuna mtu walituambia kuwa naweza kutumia unga wa dawa aina ya 'flagyl' kwa kuipaka hapo, hivyo nikawa nafanya hivyo." Anasema, huku akisisitiza haikumsaidia, bali kidonda kiliongezeka.

Ilifika hatua, baadhi ya rafiki aliyosoma nao walimchangia kiasi kidogo kilichomuwezesha kununua baadhi ya vitu vilivyohitajika, kwa ajili ya kusafisha kidonda hicho.

"Matumizi ya unga wa 'flagyl' haukuwa ushauri wa daktari aliyekuwa ananitibu awali. Kuna mtu alituambia kuwa, tukifanya hivyo kidonda kitapona, hivyo kila siku baada ya kusafishwa kidonda, walipaka unga wa dawa hiyo," anaeleza.

"Rafiki yangu ambaye nimesoma naye elimu ya sekondari siku moja alikuja kunitembea nyumbani na alipoona hali ninayopitia, huku familia ikiwa haina fedha za kunitibu, alinishauri nirekodi video fupi niombe msaada kwa wasamaria wema mitandaoni" anasema.

Mariam anaishukuru MNH kwa msaada iliyoutoa kumsafirisha kutoka Singida hadi hospitalini hapo na kumtibu bure.



Daktari Bingwa na Mkuu wa Idara ya Upasuaji katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Ibrahim Mkoma (kulia), akimfariji Mariam Rajab Juma (25), aliyelazwa katika jengo la Kibasila Wodi Namba 15, hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Ofisa Muuguzi wa Wodi hiyo, Yusta Nchemwa. **PICHA ZOTE: JOHN BADI.**

"Naishukuru sana Hospitali ya Muhimbili, kwa msaada walioutoa kwangu, Mungu awabariki sana. Wanitibu bure, wananihudumia kila kitu hadi chakula," afafanua.

**DAKTARI BINGWA**

Mtaalamu Bingwa na Mkuu wa Idara ya Upasuaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dk. Mkoma, anasema kwa kawaida kidonda chochote kinachotokea kwenye kovu la moto siyo cha kuchukuliwa wepesi, bali mhusika apelekwe hospitali kwa uchunguzi zaidi.

Pia, anasema mtu huyo anapofikishwa hospitalini, wataalam wasiishie kukisafisha kidonda, bali wachunguze kama ni cha kawaida au saratani.

"Mara nyingi vidonda vinapotokezea kwenye kovu ni saratani na mara nyingi huwa kinaanza kama kiuvimbe, halafu baadaye huwa na tabia kinapasuka na unatumia dawa hazisaidii.

"Kadri unavyokisafisha, ukikifungua unakuta kimeongezeka ukubwa kama cha Mariam.

Hivyo, hali hiyo ikizidi miezi mitatu ujue hicho siyo kidonda cha kawaida," anaelimisha.

Dk. Mkoma anasema: "Kwa historia, Mariam akiwa na umri wa miaka mitano ametusimulia kuwa aliungua moto na jeraha lilipona, ndipo miaka mitano iliyopita kikaanza tena.

"Kutokana na historia ya kidonda hiki, mara nyingi kidonda kinapotokea kwenye jeraha sugu tunachukulia kwa tahadhari, kwa sababu siyo vya kawaida, kinaweza kikawa cha kawaida au saratani."

Daktari Mkoma anasema, kutokana na utaalam, pia uzoefu alio nao, kidonda hicho siyo cha kawaida. Hivyo, walichukua sampuli na ikapelekwa maabara, waliotarajia itakayotoa majibu kama ni saratani au la.

Anasema mara nyingi aina hiyo ya vidonda, huwa ni saratani, ambayo hutokea kwenye makovu ya vidonda vilivyotokea muda mrefu uliopita.

**DADA YAKE**

Dada yake Mariam, Tatu Rajab, kwanza anaishukuru serikali kwa kutoa

# ivyomgusa JPM, nsake kwa mpigo

matibabu bure kwa mdogo wake, kwa sababu uhalisia wa maisha yao ni duni na uwezo wa kumtibu kwa hatua aliyofikia, hawakuwa nayo.

Anachangia kueleza historia ya ugonjwa wa mdogo wake, kwamba baada ya kushindwa gharama hospitalini, walikuwa wanatumia pamba na dawa na kisafisha vidonda (eusol kumsafishia ndio walimpaka dawa ya 'flagyl' wakikusudia kuua bakteria, utaalam ambao walipewa na mmoja wa madaktari huko kwao.

"Kidonda hiki kimeibuka kwa mara ya tatu. Mwanzo aliungua moto, akapona ila baada ya miaka mitano mbele likatokea jipu tukalitumbua, likashindikana kupona.

"Alipopelekwa hospitali alifanyiwa upasuaji, akakatwa nyama za paja akawekewa kwenye kidonda, akapona. Nakumbuka ilikuwa mwaka 2015," anaeleza.

Anaeleza baada ya hapo, mwezi Agosti mwaka jana kikaanza upya na kutokana na familia kukosa fedha za matibabu, wanaishia kukisafisha nyumbani hadi kufikia hatua iliyopo sasa.

"Tulikuwa tunasaga dawa hizo mbili au tatu ndipo tunampaka kwenye kidonda. Kabla ya kuugua, Mariam alipomaliza kidato cha nne, alikuwa akijihusisha na biashara ya uuzaji wa nguo," anasema.

Anamtaja kuwa ni mtoto wa nne kati



Mariam Rajabu, akiwa wodini.

ya watano, ikijumuisha wa kike wawili; baba yao ni fundi ujenzi na mama ni mzazi nyumbani.

**WAZIRI UMMY**

Waziri Ummy anasema, baada ya kuona video hiyo mtandaoni, walizungumza na Ofisi ya Mkoa wa Singida, iliyomtafuta na kumpata kwa taratibu za kupelekwa hospitali ya Muhimbili, kwa ajili ya matibabu.

"Jambo hili pia lilimgusa Rais Dk. John Magufuli na yeye alinitumia ujumbe wa simu na picha ya huyu mtoto akasema tumsaidie. Wakati Rais ameguswa, tayari taratibu za kumsaidia zilikuwa zimeshaanza," anasema.

Waziri anawashauri Watanzania wasichelewe kufika kwenye vituo vya kutoa huduma za afya, pindi wanapopata changamoto za magonjwa.

"Mgonjwa anafika hospitali ugonjwa ukiwa kwenye hatua za juu zaidi. Hili ni tatizo ambalo naliona sana, mgonjwa anakaa miaka hadi miwili nyumbani hadi ugonjwa umefika hatua ya juu zaidi, ndipo anapoomba msaada. Hii inafanya matibabu yawe na changamoto," anasema.

Waziri Ummy anatoa wito kwa wananchi kukata bima za afya, kwa sababu matibabu ni gharama kubwa. Anafafanua: "Sasa hivi tuna bima za afya za CHF ambazo matibabu yanakufikisha kwenye Hospitali za Rufani za Mkoa kwa Sh.30,000 tu."

Pia, waziri anasema kuna Sera ya Afya inayosimamia utoaji huduma za afya na asiye na uwezo wa kuchangia huduma, anatakiwa kufuata taratibu kupitia Ofisi za Ustawi wa Jamii katika hospitali husika, watakaomwandikia barua itakayomtambulisha haki ya kupatiwa huduma bure.

"Upo mfumo mzuri na ni jukumu la serikali kuhakikisha Watanzania wasio na uwezo wanapata huduma za matibabu bila kikwazo cha cha fedha. Ndio maana tunaenda kwenye bima ya afya, ili iwe rahisi kupata huduma bila kikwazo cha fedha,"anafafanua.

**MUHIMBILI HOSPITALI**

Mkuu wa Mawasiliano kwa Umma na Huduma kwa Wateja Hospitalini wa MNH, Aminiel Aligaesha, anasema matibabu ya Mariam yanagharamiwa na serikali na yeyote atakayetaka kumsaidia kwa ajili ya mambo mengine, utaratibu utatolewa baadaye.

"Ninajua wapo wadau wengi ambao wameguswa na matibabu ya Mariam, ila tunaomba kuwaeleza kuwa serikali imebeba matibabu yake yote.

"Kama kuna mtu atataka kumsaidia kutokana na namna alivyojieleza awali kuwa familia yake ni maskini, muda ukifika mtatangaziwa utaratibu namna ya kumsaidia," anafafanua Aligaesha.

# Lijue jeraha sugu, sura zake kuu nne

JERAHA sugu; tafsiri yake ni kidonda kisichopona katika utaratibu uliojipanga na katika kiasi cha muda unaotabirika, kama ilivyo kwa majeraha mengi.

Majeraha yasiyopona ndani ya miezi mitatu, mara nyingi huchukuliwa kuwa sugu. Kwa mfano, majeraha sugu hubaki katika hatua ya uvimbe kwa muda mrefu sana.

Ni majeraha yanayosababishia wagonjwa, dhiki kali za kimwili na kimawazo, pamoja na kugeuka mzigo mkubwa wa kifedha kwa wagonjwa na mfumo mzima wa huduma ya afya.

**AINA ZAKE**

Idadi kubwa ya majeraha sugu inagawanywa katika makundi matatu: Vidonda vya vena; vidonda vya kisukari, na vidonda mvuke.

Kuna idadi ndogo ya majeraha ambayo hayapo katika makundi haya makuu. Inaweza kuwa inatokana na sababu kama vile sumu ya mionzi au shida ya damu kusafiri kwenda sehemu fulani ya mwili.

**VIDONDA VENA AU ATERI (MISHIPA)**

Vidonda vya vena, ambavyo kwa kawaida hutokea miguuni, inaelezwa vinachangia kati ya asilimia 70 hadi 90 ya majeraha sugu, inaathiri wazee zaidi.

Inadhaniwa, chanzo zaidi kikubwa ni kutokana na vena (mishipa) kutofanya kazi vizuri na kuzuia damu kupita ipasavyo.

Shida ya damu kusafiri kwenda sehemu fulani ya mwili hutokea, huku kunakuwapo uharibifu wa mishipa inayofikia katika majeraha.

**VIDONDA KISUKARI**

Sababu nyingine kubwa ya majeraha sugu, ni ugonjwa wa kisukari, Wagonjwa hao wana hatari kwa zaidi ya asimia 15, pindi mwili unapodhurika kama vile kukatwa.

Kisukari husababisha ugonjwa mwingine uitwao pathi, ambao unazuia mtu kutambua au kuhisi maumivu mwilini. Hivyo, wagonjwa wanaweza wakakosa kuyaona majeraha madogo miguuni, pindi anapojeruhiwa tena.

Aidha, kisukari husababisha kupungua kinga na uharibifu wa mishipa midogo ya damu, pia inauzuia uwekaji oksijeni wa kutosha kwenye mishipa midogo (tishu), inayoweza kusababisha majeraha sugu.

**VIDONDA SHINIKIZO**

Aina nyingine inayoongoza ya majeraha sugu ni vidonda vya shinikizo, ambavyo kwa kawaida hutokea kwa watu walio na hali kama vile kupooza, matatizo yanayohusiana na nyendo au mshituko wa moyo.

Hiyo inazuia damu kusonga kwa sehemu katika baadhi za sehemu za mwili, ambazo kwa kawaida huwa na shinikizo kama vile visigino.

Vidonda vya shinikizo, husababishwa na kupungua damu inayoingia kwenye baadhi ya sehemu za mwili.

**ISHARA/DALILI**

Mara nyingi wagonjwa wa majeraha sugu hulalamika kuwa na maumivu makali katika sehemu kubwa katika maisha yao.

Inashuariwa kwamba, watoa huduma za afya, kukabiliana na maumivu yanayohusiana na majeraha ya muda mrefu, kama moja ya vipaumbele katika usimamizi ya kuhudumia majeraha hayo sugu.

Takwimu zinabainisha wagonjwa sita kati ya 10 wa vidonda sugu wanalalamika maumivu makali. Ni maumivu yanayoendelea hata usiku au wakati shughuli zote zimetulia.

**Makala hii ni kwa mujibu wa mtandao.**

# MAJINA YA VIMBUNGA YANAKOTOKEA

## ■Pata simulizi ya Kenneth iliyopinda kona



Maeneo mbalimbali yaliyoathiriwa na vimbunga. Chini, kimbunga Kenneth ilivyokuwa Comoro. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



WIKI hii Watanzania hasa walioko katika ukanda wa Pwani ya Kusini mwa nchi, walikuwa katika hofu kubwa kuhusu ujio wa kimbunga ambacho kilitabiriwa kuwa na madhara katika siku kadhaa.

Hofu na taharuki imetawala hasa katika mikoa ya Mtwara na Lindi, kwamba lolote baya laweza kutokea.

Kasi ya kumbunga hicho chenye upepo mkali wa kasi ya kilomita 220 kwa saa, kimesababisha vifo vya watu watatu katika visiwa vya Comoro, ambako ndiko kilikoanzia.

Idara ya kitaifa ya kukabiliana na majanga nchini Msumbiji, inaeleza kwamba takriban watu 30,000 walihamishwa kutoka maeneo yaliyotarajiwa kuathirika na kimbunga hicho.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imenukuliwa kwamba kimbunga cha mwisho kuikumba nchi hiyo, kilikuwa mwaka 1952, huko mkoani Lindi. Ni miaka 66 sasa.

"Wakati kule Lindi haikuwa na watu wengi na wala hakukuwa na miundombinu mingi ya kuharibiwa, kama ilivyo kwa sasa," anasema Dk. Agness Kijazi Mkurugenzi Mkuu wa TMA.

Jana mchana akizungumza, Dk. Kijazi, alisema tishio lililokuwapo kuhusu kimbunga nchini, limeondoka, kwani kimbunga kimebadili mwelekeo baharini, watu waendelee na shughuli zao, lakini muhimu ni kukaa kwa tahadhari.

### MAJINA YAKE

Umewahi kusikia vimbunga vikiwa na majina ya kushangaza na sababu za kuitwa hivyo? Kipo ilichoitwa Idai, ambacho kilisababisha uharibifu mkubwa katika baadhi ya maeneo ya nchi za Msumbiji, Malawi na Zimbabwe.

Ni hivi karibuni, Umoja wa Mataifa umesema, huenda likawa ndilo janga baya zaidi la hali ya hewa kuwahi kushuhudiwa, Kusini mwa Afrika.

Pia, kuna kimbunga Matthew, kilichokumba nchi za Haiti, Jamaica, Jamhuri ya Dominika, Bahamas na baadhi ya majimbo ya Marekani, mwezi Oktoba, 2016.

Mwezi mmoja kabla, kimbunga kingine kilichojulikana kwa jina la Hermine, kilisababisha uharibifu mkubwa katika jimbo la Florida, Marekani.

Lakini, kinachokumbukwa sana huko Marekani, kuna kimbunga Katrinam, ambacho kiliathiri sana majimbo ya Louisiana, Mississippi na Alabama

### MAJINA YANAKOTOKEA

Vimbunga katika maeneo ya bahari ya Atlantiki, Caribbean na Ghuba ya Mexico, hupewa majina kutoka Shirika la Utabiri wa Hali ya Hewa Duniani (WMO), lenye makao makuu, nchini Uswisi.

Zamani, ni majina ya kike pekee yaliyotumiwa na baada ya kuanzia mwaka 1979, majina ya kiume yalianza kutumiwa.

Huwa kuna makundi sita ya majina ambayo hutumiwa kwa mzunguko. Hii ina maana kwamba majina yaliyotumiwa kwenye vimbunga mwaka hu hayatatumiwa tena hadi 2022.

Majina yaliyoko kwenye orodha hiyo, yanaweza kubadilishwa na WMO. Ni orodha iliyoanza kutumiwa mwaka 1979.

Kabla ya hapo, jina la kimbunga Fern lilibadilishwa mwaka 1966 na badala yake kukatumiwa Frieda. Hakuna sababu iliyotolewa.

### MAJINA YALIYOTELEKEZWA

Baadhi ya majina huacha kutumiwa, hasa kunapotokea uharibifu mkubwa au hasara kubwa, katika mtazamo kutumia tena jina hilo, maana yake ni kufufua kumbukumbu zenye uchungu.

Mfano hai, unatajwa ni kimbunga Katrina kilichoua watu 2,000 mwaka 2005 na kusababisha uharibifu mkubwa nchini Marekani, kikiwaacha watu milioni moja bila makazi. Miji ya New Orleans na Louisiana iliathirika.

Ndani ya WMO, kuna kundi la wataalamu liitwalo Kamati ya Vimbunga vya Tropiki, ambalo hukutana kila mwaka, ndilo linaloamua ama majina yatakayotumika tena au yataachwa.

### MAJINA YALIYOACHWA

Ukiondoa Katrina, kuna majina mengine yaliyoachwa kutumiwa. Hilo ni Mitch, kutokana na kimbunga cha mwaka 1998, kilichoua watu 11,000 walioko Honduras na Nicaragua, jina halitumiwi tena.

Kimbunga hicho ndicho kibaya zaidi kukumba maeneo ya Magharibi mwa dunia katika kipindi cha miongo miwili iliyopita.

Kimbunga Sandy cha mwaka 2012 na Kimbunga Irene 2011, pia vilisababisha uharibifu mkubwa. Majina hayo hayatumiwi tena.

Kimbunga hatari zaidi kuwahi kuikumba Marekani, kilitokea mwaka 1780 na kiliua watu 22,000 maeneo ya Martinique, Barbados na St Eustatius. Wakati huo majina hayakuwa yameanza kutumiwa kurejelea vimbunga.

### MAJINA YAACHWA 1954

Katika maeneo, kuna jedwali la majina ya vimbunga. Inapotolewa jina na linapotokea lingine, kimbunga kinachofuata hupewa.

Kwa mfano, kimbunga cha kwanza Cambodia kilipewa jina la Damrey na kitakachofuata, kilipewa jinala Kaikui, huko China.

Kimbunga cha sasa maeneo hayo, nchini Thailand, inaitwa Chaba. Kupitia mfululizo huo, kilitwa hivi karibuni Megi, ambacho kiliathiri nchi za China na Taiwan. Jina hilo la nne, huko Korea Kusini.

Majina ya vimbunga na tufani, yalianza kutumiwa nchini Uingereza na Ireland, kwa majaribio. Kuna wakati majina yanayotolewa kupitia alfabeti, isipokuwa; Q, U, X, Y na Z, ambao ndio utaratibu unaotumiwa kuvipa majina vimbunga Atlantiki Kaskazini.

### MUHTASARI WA KENNETH

■Kimbunga Kenneth kilijitengeneza Kaskazini mwa Madagascar

■Jumatano kilipita kwenye visiwa vya Comoro

■Watu watatu wamethibitishwa kupoteza maisha Comoro

■Kimetua mkoa wa Pemba kaskazini mwa Msumbiji.

■Mpaka sasa hakuna athari zilizoripotiwa Mtwara, Tanzania

■Bado hakuna taarifa rasmi juu ya hali ya maafa Msumbiji

■Kasi imepungua ya kimbunga Kenneth na upepo wake, hata hivyo mvua kubwa bado inatarajiwa.

**Makala hii inatokana na taarifa za mtandao.**

HABARI KIMATAIFA

# Kim Jong-Un aishutumu Marekani kupotosha ukweli

**VLADIVOSTOK,** Urusi

KIONGOZI wa Korea Kaskazini, Kim Jong-Un, ameishutumu Marekani kwa kupotosha ukweli wakati wa mkutano uliofanyika mwanzoni mwa wiki kati yake na Rais Donald Trump.

Kim amesema kwamba amani katika rasi ya Korea itategemea utawala wa Washington. Aliitoa kauli hiyo alipokutana na Rais wa Urusi Vladimir Putin katika mji wa Vladivostok.

Kim alimweleza Rais Vladimir Putin kwamba hali katika rasi ya Korea na kanda hiyo kwa ujumla bado ni tete na imefikia wakati mgumu.

Kim (pichani chini) alionya kuwa hali inaweza kurejea mahali ilipokuwa kwa sababu Marekani imeamua kuchukua mkondo wa kupotosha ukweli wakati wa mazungumzo yao yaliyofanyika hivi karibuni. Hali hiyo imekuja ikiwa imepita wiki moja baada ya kuishutumu Marekani kuvuruga mazungumzo ya amani.

Mazungumzo baina ya nchi hizo mbili yalivunjika wakati wa kikao cha Vietnam kilichofanyika Februari, bila kufikiwa kwa mkataba juu ya silaha za nuklia za Korea kaskazini.

Mazungumzo hayo yaliripotiwa kukwama kutokana na madai ya Korea Kaskazini kudai kuondolewa vikwazo kamili vya kiuchumi ndio iweze kuahidi kuachana na silaha hizo, mkataba ambao Marekani haiko tayari kuukubali.

Kwa mujibu wa msemaji wa Rais wa Urusi, Dmitry Peskov, utawala wa Kremlin unaamini mazungumzo yanayohusisha pande sita juu ya Korea kaskazini, ambayo kwa sasa yamekwama, ndio njia inayofaa kutatua suala la silaha za nyuklia katika rasi ya Korea.

Mazungumzo hayo yaliyoanza mwaka 2003, yanazihusisha Korea kusini na kaskazini, China, Japan, Urusi na Marekani.

Ziara hiyo inaangaliwa kwa kiasi kikubwa kama fursa kwa Korea Kaskazini kuonyesha kuwa inashirika wenye nguvu baada ya mazungumzo na Marekani mapema mwaka huu kukwama.

Nchi hiyo imemlaumu Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo kwa kuvunjika kwa mkutano huo. **BBC**



# Wahukumiwa kunyongwa kwa kumuua askofu

**CAIRO,** Misri

WATAWA wawili wa kiume wa Kanisa la Khufti (Coptic), wamehukumiwa kifo nchini Misri kutokana na kuhusika katika mauaji ya askofu mwaka 2018.

Askofu Epiphanius (64), alipatikana akiwa ameuawa huku akivuja damu nyingi ndani ya makazi ya kanisa kaskazini magharibi mwa Jiji la Cairo Julai 2018.

Mamlaka za Misri zilihusisha tukio hilo na ugomvi ambao haukuwekwa wazi baina ya watawa hao na askofu Epiphanius.

**Mamlaka za Misri zilihusisha tukio hilo na ugomvi ambao haukuwekwa wazi baina ya watawa hao na askofu Epiphanius.**

Hukumu ya kunyongwa dhidi ya watawa hao ilipitishwa Februari mwaka huu na kisha kupelekwa kwa mufti mkuu wa Misri ili kupitishwa.

Jumatano wiki hii, Mahakama ya Damanhur ilithibitisha kuwa hukumu dhidi ya watawa hao imepitishwa.

Mmoja wa watawa hao, Wael Saad, anaripotiwa kukiri mbele ya waendesha mashtaka kuwa alitumia nondo kumshambulia askofu huyo mpaka kufikwa na umauti.

Mtawa mwengine, Remon Rasmi, alishtakiwa kwa kosa la kumpatia Saad usaidizi.

Saad and Rasmi, ambao pia walikuwa wakifahamika kwa majina yao ya kikanisa ya Ashiah na Faltaous, wanaweza kukata rufaa dhidi ya hukumu hiyo.

Idadi ya wafuasi wa kanisa hilo wanafikia asilimia 10 ya raia wote wa Misri.

Baada ya mauaji hayo, kiongozi wa kanisa hilo, Papa Tawadros II, alitangaza hatua mbali mbali zilizolenga kurejesha nidhamu baina ya watumishi wa kanisa.

Pia alisitisha uandikishaji wa watawa wapya kwa kipindi cha mwaka mzima, watawa wote wametakiwa kufunga kurasa zao zote za mitandao ya kijamii.

Wakhufti walijitenga na madhehebu mengine ya kikristo mwaka 451, hivyo ni moja ya makanisa makongwe zaidi duniani.

Kanisa hilo ndio kubwa zaidi katika Mashariki ya Kati, na pia lina wafuasi zaidi ya milioni moja nje ya Misri. **BBC**




Barabara katika Jimbo la Delgado nchini Msumbiji, ikiwa imeharibika kutokana na athari ya Kimbunga Kenneth ambapo mtu mmoja amefariki. **PICHA: AP**

# Kimbunga Kenneth chaacha maafa

**MAPUTO,** Msumbiji

KIMBUNGA Kenneth kimepiga pwani ya kaskazini ya Msumbiji huku mvua kubwa zikitarajiwa kunyesha mara mbili zaidi ya dhoruba iliyoupiga mji wa Beira mwezi uliopita.

Mtu mmoja amefariki huku makazi ya wananchi wengi yakiharibiwa kutokana na upepo mkali ulioambatana na mvua.

Kimbunga Kenneth kimelipiga jimbo la Cabo Delgado, kisha baadae kikaelekea jimbo la Sofala kaskazini mwa Msumbiji ambako ndiko uliko mji wa Beira ulioathiriwa zaidi na kimbunga Idai mwezi uliopita.

Kwa mujibu wa shirika la Mpango wa chakula la Umoja wa Mataifa (WFP), kimbunga Kenneth kinatarajiwa kusababisha mvua kubwa katika kipindi cha siku 10 zijazo ikiwa ni mara mbili zaidi ya zile zilizonyesha wakati wa kimbunga Idai.

Katika taarifa yake WFP imesema wilaya nne za Cabo Delgado, Macomia, Mocimboa da Praia, Muidumbe na Palma, zinatarajiwa kuathirika zaidi kutokana na upepo unaotarajiwa kupiga kwa zaidi ya kilometa 120 kwa saa.

Kwa mujibu wa WFP, watu 112,000 wako hatarini na kwamba shirika hilo lina zaidi ya tani 1,000 za msaada wa chakula tayari kuwasaidia watakoathirika.

Serikali ya Msumbiji imeanza kuwalazimisha watu kuondoka katika maeneo yaliyoko hatarini siku mbili kabla ya kimbunga kupiga.

Watu 30,000 wamehamishiwa katika maeneo salama, huku shule zikitumika kuwahifadhi watu hao.

Rais wa Msumbiji Filepe Nyusi, amewahutubia wananchi kupitia televisheni akiwataka kuwa watulivu.

Kimbunga hicho pia kilisababisha maafa katika visiwa vya Comoro.

Mkurugenzi mkuu wa ulinzi wa kiraia visiwani humo, Ismael Mogne Daho, alithibitisha vifo vya watu watatu.

"Usiku ulikuwa wa hofu sana matumboni mwetu. Kuanzia saa nne usiku na kuendelea, hatukulala. Hali ya hewa ilikuwa mbaya sana na hatukujua wapi pa kwenda katika kiza cha namna ile na watoto. Mvua kubwa ilinyesha na upepo mkali. Miti ilianguka, hapo palikuwa na muembe, tulikuwa tukikaa chini yake lakini uliangushwa" alisema Daho.

Mkuu wa shirika la misaada ya binadamu la Umoja wa Mataifa (OCHA), Mark Lowcock alisema upepo unaotokana na kimbunga Kenneth umefikia kilometa 270 kwa saa na kusababisha mafuriko makubwa.

Naye Naibu Mkurugenzi katika taasisi ya kupambana na maafa ya Msumbiji, Antonio Beleza alisema kuwa asilimia 90 ya nyumba katika kisiwa cha Ibo mjini Cabo Delgado zimeharibiwa na dhoruba.

Mwanamke mmoja ameripotiwa kupoteza maisha katika mji wa Pemba kaskazini mwa Msumbiji baada ya kuangukiwa na mti kutokana na kimbunga hicho, huku nyumba zikiharibiwa. **DW**

# HADITHI

AJALI kubwa iliyotikisa nchi inatokea eneo la Mikese mkoani Morogoro baada ya basi la abiria kuungua moto, kuua na watu wengine kujeruhiwa. Awali inachukuliwa poa kama ajali za kawaida. Lakini nyuma ya pazia ni ajali iliyopangwa na muuaji, mwenye akili za kiwendawazimu, akibebwa na hisia za chuki, wivu na kisasi bila kujali madhara kwa watu wengine wasiohusika. Eddy Kamal, mpelelezi makini, anategua kitendawili hiki. Fuatilia kisa hiki....

# KISANDUKU CHEUSI - **45**

**Na Adam Fungamwango**

"Kazi nzuri sana Eddy, nchi itaendelea kukukumbuka na kukuenzi kwa kazi kubwa unayoifanya."

Jina la Eddy lilimshtua Mapunda. Alishangaa kuona bosi yule akitamka jina la Eddy kwa askari yule mpelelezi aliyeishi naye kwenye jengo lake kwa wiki nzima.

Aligeuza kichwa chake na kutazama tena Eddy. "Kumbe huyu ndiye Eddy?" Alijiambia mwenyewe.

Alijikuta akianza kutetemeka mwenyewe. Pamoja na kukamatwa, lakini alidhani kuwa alicheza na askari mpelelezi wa kawaida.

Kumbe alikuwa ni Eddy. Mpelelezi ambaye hajawahi kumuona kwa sura, lakini habari zake hakuna mtu asiyezijua. Ni mmoja wa wapelelezi hodari na hatari si tu Tanzania, bali Afrika nzima.

Anakumbuka jinsi alivyokuwa akisoma kwenye magazeti jinsi alivyoweza kukabiliana na mikasa mingi ya ajabu, lakini na kuibua mambo mazito yaliyojificha yanayopangwa na maadui wa taifa.

Alidhani alimteka Mayambua ili amuue, kumbe alikuwa amemteka Eddy. Lilikuwa ni kosa kubwa sana maishani wake.

Alizidi kujutia uamuzi wake. Wakati akipanga kulipua basi kwa ajili ya kumuua Careen, hakujua kama mambo yatakuwa makubwa kiasi cha kuingiliwa na mpelelezi mkubwa kama huyo.


Pamoja na kukamatwa kwake, kimoyomoyo alimsifu na kukubali kuwa ni mpelelezi makini na anayeijua kazi yake vema kwa sababu kama ingekuwa ni mpelelezi wa kawaida, asingepata kitu na pia angeweza kumuua kwa jinsi alivyojipanga.

Akiwa kwenye pingu, Mapunda na mabaunsa wake wawili waliobaki hai, walipandishwa kwenye gari maalum la serikali, Land Cruiser kupelekwa sehemu maalum kwanza kwa ajili ya mahojiano, kabla sheria kufuata mkondo wake.

Baadhi ya walinzi wa jengo hilo waliokamatwa waliingizwa kwenye lori, Mwakabana alipanda gari yake, huku Eddy akipanda gari ya ofisini kwake iliyokuwa ikiendeshwa na sekretari wake, Lilly.

"Lilly, nashukuru kukuona tena, na pia nashukuru kwa kufikisha maagizo yangu inavyopaswa, wewe ni mwanamke wa shoka na umeshiriki katika sakata hili la kuwatafuta watu ambao wamewadhulumu maisha wanawake wenzako, unafaa uenziwe." Eddy alimmiminia sifa Lilly.

Lilly kwa upande wake hakujua kama afurahi, alie au acheke.




**Du yaani demu anakukataa unamuua? Si unatafuta mwingine, wanawake wote hawa bado unafanya mchezo huo wa kitoto, ona sasa imekamatwa.**

Ni kweli sifa alizotoa Eddy zilimpasa, lakini aliona ni moja kati ya kazi yake aliojiriwa na analipwa na kazi hiyo.

"Nashukuru sana bosi, lakini kuna kitu nahitaji zaidi kwako kuliko sifa hizi." Alisema huku akiitafuna lami kuelekea Kijitonyama, nyumbani kwa Eddy ambako alimtaka waende kwanza akabadilishe nguo.

"Najua, leo hii hii nakutoa auti."Eddy alisema huku akimtazama Lilly ambaye alibinua mdomo wake akitabasamu, lakini pia lilikuwa ni kama vile haamini.

Sifa za Eddy, uwezo walionao wa mapigano, historia yake, wajihi, ucheshi na uwezo mkubwa wa kuzungumza, ulimfanya kupendwa na watu wengi wakiwemo akinadada.

Ilimfanya kuandikiwa barua, email na waraka mbalimbali wa mapenzi, huku akipokea wageni wengi afisini kwake wakiwemo warembo kutoka nchi mbalimbali duniani.

Kama binadamu, hali hii ilimfanya Lilly naye kuingiwa na wivu akitaka kujua ni kwa nini bosi wake amekuwa ni sukari ya warembo.

"Kila siku huwa unanidanganya utanitoa auti, haya bwana kwa sababu mimi siyo mrembo, sisi vinyago vya mpapure tukiongozana tutachafua gazeti." Mara kwa mara alikuwa akimwambia Eddy kwa namna ya kumtania bosi wake, lakini ulikuwa ni utani ambao una ukweli ndani yake.

"Usiwe na wasiwasi bibie, hao unaosema warembo tena wenye sifa za kukaa kwenye kiti ulichopo lakini hawapo, uko wewe hapo. Na hata hivyo wewe si mwanamke mbaya kama unavyojieleza, ipo siku nitakuonyesha kuwa wewe ni moja ya wanawake bora kabisa na hutorudia tena sentesi hiyo." Eddy huwa anamjibu.

Lilly alipaki gari nyumbani kwa Eddy, akashuka na kumwambia aende nyumbani wake anajiandae ili wakutane saa moja usiku kwenye hoteli ya Cassanova iliyopo Ilala jijini Dar es Salaam.

"Wewe nenda na gari yangu kalale, fanya shughuli zako, mimi nitakuja mwenyewe Ilala, wewe nenda na gari yangu usinifuate." Alimwambia huku akimbusu. Ilikuwa yapata saa nane usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

*********************************

Ndani ya hoteli ya Cassanova kulikuwa na watu wengi. Wengine walikuwa wakipata vinywaji taratibu. Wengine walikuwa wakicheza muziki sehemu ambayo ilikuwa imetengwa kwa ajili hiyo.

Siku hiyo hoteli ilipokea pia wateja wawili. Eddy na Lilly walikuwa wamekaa kwenye kona ya pembani inayotazama mlango mkuu.

Tayari Lilly alikuwa ameshakunywa bia kadhaa ambazo zilimfanya kulala kwenye mapaja ya Eddy.

Kwa upande wake Eddy hakuwa mnywaji sana. Mpaka wakati ule alikuwa ameshakunywa bia mbili tu na alikuwa na mpango wa kugiza ya tatu amalize kazi.

Na huwa anakunywa kwa ajili ya kampani tu, kwa kawaida hakuwa yule mtu wa kila siku yeye yuko baa.

Wakati mwingine ukimuona baa au kwenye mahoteli sehemu za vinywaji ni kwa ajili ya kazi yake. Mara taarifa ya habari kwenye televisheni yake ikaanza.

Kila mmoja, hata wale aliokuwa wakicheza ovyo na kupiga kelele waliacha ili kusikiliza nini kimejiri.

'Polisi nchini wamemkatana Mkurugenzi Mtendaji na mmiliki wa hoteli ya Paradiso Benson Mapunda na wenzake kwa tuhuma za kulipua basi la abiria la Bomoa Trans na kuuza zaidi ya wati 10 na majeruhi zaidi ya 20.

Ajali hiyo ilitokea miezi sita iliyopita kule Mikese na kudhaniwa kuwa iliungua kutokana na tatizo la injini kabla ya kuwaka moto, imebainiwa kuwa ilikuwa hujuma ya Mapunda na watu wake.

Taarifa zinasema kuwa Mapunda alimtuma mtu wake aliyekuwa amebeba 'breafcase' iliyokuwa ina bomu ndani na ndiyo iliyotumika kulipua basi hilo.

Mtuhumiwa pia anadaiwa kufanikiwa kuua watu wengine wawili, Hellen na Said kwa ajili ya kuficha uovu wake.

Ushahidi wa awali unaonyesha kuwa mtuhumiwa alifanya hivyo kwa hasira baada ya mchumba wake wa siku nyingi Careen kuamua kumuacha na kutaka kuolewa na mtu mwingine.

Imedaiwa kuwa Careen alikuwa ndani ya basi hilo akitoka Dar es Salaam kwenda Ifakara kwa ajili ya harusi yake, lakini hafika baada ya Mapunda kutekeleza mpango huo wa kukatisha maisha yake kabla hajaolewa.

Ni yule yule kijana mzalendo wa Kitanzania, Eddy Kamal, alibaini mpango huo na kuupeleleza kwa kina na kuibua kila kitu kilichojificha.

Kwa sasa mtuhumiwa pamoja na wenzake wapo kizuizini na wanatarajia kufikisha mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.' Ilimaliza taarifa hiyo.

Picha za televisheni zilimuonyesha Kamanda na Polisi, pamoja na watuhumiwa wote.

"Huyu Eddy kiboko, yaani kila tukio tata, ujue yeye yumo." Alisikika mtu mmoja aliyekuwa karibu na meza ya Lilly na Eddy mwenyewe.

Wengi walionyesha kushangaa na kusikitika kwa wakati mmoja.

"Du yaani demu anakukataa unamuua? Si unatafuta mwingine, wanawake wote hawa bado unafanya mchezo huo wa kitoto, ona sasa imekamatwa." Mtu mwingine alidakia kwenye meza nyingine.

Kwa bahati nzuri hakukuwa na picha yoyote ya Eddy iliyoonyeshwa kama ilivyo kawaida.

Hata siku moja hakutaka picha yake ilichapishwe kwenye gazeti au kuonyeshwa kwenye televisheni kwa sababu ya usalama ili iwe rahisi kwake kuendelea na kazi yake kwa ufanisi.


Wote hawakujua kama mtu aliyekuwa akisifiwa yumo mle ndani.

Mwenyewe Eddy alikuwa na furaha moyoni baada ya kumaliza kazi kubwa iliyokuwa inamkabili.

Hata hivyo, moyo wake bado ulikuwa ukimuuma kutokana na kumpoteza Hellen, msichana aliyempenda, pacha wa Careen, lakini akauawa kutokana na kuonekana kutaka kuitoa siri ya kifo cha pacha mwenzake kwake.

*Itaendelea Jumamosi*

## KATUNI


MVURUGO WA WIKIENDI
NA MUHIDINI MSAMBA
INACHOMA
MTAKALIA KUSEMA NINABEBWA HIVYO HIVYO MWENYEWE NAJILIAGA
WATABIRI WANASEMA KUWA SHUTI LA PENATI LA YULE DOGO BOKO BADO LIPO HEWANI HIVYO INABIDI TUWE NA TAHADHARI
WEWE WA WAPI,MPIRA UMEONEKANA MWANZA
KIJIWE
ETI ZISI IS MNYAMA WENYEWE MNABANA PUA MARA KIKOSI KIPANA, MARA WA KIMATAIFA MNGEKUWA NA SIFA ZOTE HIZO SI MNGE MPIGA MAGOLI MENGI MTOTO WA KINONDONI
HEHEHEHE... LABDA KWA KUBEBWA NA WAAMUZI WA BONGO
SAWA SISI TUMEBEBWA MBONA YENU HAMSEMI, WACHEZAJI WENU KUGOMA SABABU YA NJAA
HIVI NI KWELI IPO NANE BORA AFRIKA AU BORA NANE AFRIKA YAANI KWA MPIRA HULE HATA UMISHUTA HAWASHINDI LABDA WABEBWE
HATA HAJIBU IMEMSHINDA HELE YA KUNYOLEA NDEVU!?
WENZENU TUNAJICHANGISHA WENYEWE HATUTEGEMEI MTU AFURAHI NDIO TULE PILAU
KIBANDA UMIZA
MAKAVU MUBASHARA
LEO UTANIONYESHA MCHEPUKO ULIOSEMA MBELE YA MKULU
MKE WANGU NILIKUWA NATANIA TU ILI NIMFURAHISHE MKULU
RC MB
SIKUELEWI KABISA YAANI TUNASHINDIA BAMIA NA KAUZU WEWE UNACHEPUKIA MSHAHARA!?
CHONDE MKE WANGU USINIPE TALAKA
ACHA HIZO
WAIFU LEO SITOWEZA KURUDI KWANI TUPO BIZE KUFATILIA HULE MPIRA WA PENATI ULIOPIGWA NA DOGO WA MSIMBAZI UTAANGUKIA WAPI ILI USILETE MADHARA
USINIFANYE MJINGA SASA KWA TAARIFA YAKO UMEONEKANA MWANZA TENA YEYE MWENYEWE KAUONYESHA
DU! ISHAKUWA SOO

# POGBA ATABAKIA MAN UTD - SOLSKJAER




**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer anatarajia Paul Pogba kubaki Manchester United licha ya Real Madrid kujiamini kwamba wanaweza kumsajili kiungo huyo.

Pogba amekuwa akishutumiwa kwa kuwa kwenye kiwango kibovu wakati Manchester United ikitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kutokuwapo kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu.

"Huwezi kuwa na uhakika wa kila kitu kwenye soka, lakini nafikiri Paul atabaki hapa," alisema Solskjaer.

"Naweza kuwahakikishia kwamba, kwa sasa akili yake ipo hapa na anataka kupata mafanikio akiwa na Man United.

"Siwezi kusema kwa uhakika, lakini kwenye maisha huwezi kusema kamwe. Ninachojua ni kwamba atakuwa na sisi hapa.

P"ogba anabakia kuwa 'kiongozi' kwenye chumba cha kubadilishia nguo.

"Dunia imebadilika, huna Bryan Robson, Roy Keane au Steve Bruce kwenye vyumba vya kubadilishia nguo," alisema Solskjaer.

## Sarri apigwa faini na FA

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri, amekubali adhabu aliyopewa na Chama cha Soka cha England, FA, kwa utovu wa nidhamu wakati wa sare yake na Burnley kwenye dimba la Stamford Bridge Jumatatu usiku.

Sarri amepigwa faini ya pauni 8,000 baada ya kukubali kosa lake ambalo alishitakiwa na FA.


Katika taarifa yake rasmi, msemaji wa FA kupitia ukurasa wa Twitter alielezea: "Maurizio Sarri amepigwa faini ya pauni 8,000 baada ya kukubali kufanya kosa la utovu wa nidhamu na amekubali adhabu yetu.

"Ni kutokana na tabia yake na kutolewa nje kwenye dakika ya 94 katika mchezo kati ya Chelsea na Burnley katika mchezo wa Ligi Kuu."

Hata hivyo, Msaidizi wa Sarri, Gianfranco Zola, ambaye alichukua majukumu ya kocha huyo mwenye umri wa miaka 60, alibainisha kwamba Muitaliano mwenzake huyo alichokozwa na benchi la ufundi la Burnley.

Alisema Sarri alichukizwa na kitendo cha uchokozi wa benchi la ufundi la Burnley.

Akizungumzia tukio hilo, Zola alielezea: "Alikasirika, hivyo alikua akiwafuata kwenye bechi lao na akatolewa nje."






## *Zidane: Ubingwa La Liga unatuhusu msimu ujao*

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane amesema kwamba kipaumbele cha Real Madrid msimu ujao ni kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga.

Ushindi wa Barcelona dhidi ya Alaves ulithibitisha Madrid hawawezi kuwa kwenye mbio za ubingwa huo baada ya kuwa nyuma kwa pointi 16 na miamba hao wa Katalunya.

Licha ya kuwa na mafanikio kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, inamaanisha kwamba Madrid imeshinda taji hilo mara moja ndani ya miaka saba iliyopita, huku Barca ikishinda mara nne kwa kipindi cha miaka minne iliyopita na mara nane kwa kipindi cha misimu 11.

"Kipaumbele chetu mwakani ni kutwaa ubingwa wa ligi," alisema Zidane akinukuliwa na Sky Sports.

"Ni mashindano ya muda mrefu, ni moja kati ya mataji ambayo hutakiwi kuyakosa na nitawaambia wachezaji hicho ndicho kipaumbele chetu.

"Hilo litakuwa na mkazo mkubwa zaidi kwetu na wachezaji wote watatakiwa kulijua hilo, maana Kombe la Ligi ndiyo kitu muhimu zaidi kuliko mataji mengine."

Barcelona kutwaa taji lao la 26 kutathibitishwa kwenye mchezo wao unaokuja kama ikishinda.

"Tuna mataji 33," alisema Zidane. "Barca wanafanya vizuri, lazima nikubali kwamba wapizani wetu wanafanya vizuri kwa sasa, lakini katika historia Real Madrid wana mataji mengi zaidi."

# Mourinho ‘kaua’ kila mtu Real – Adebayor

**LONDON,** England

EMMANUEL Adebayor amedai kwamba Jose Mourinho “alimuua kila mtu” kwenye vyumba vya kubadilishia nguo vya Real Madrid, akiwamo Cristiano Ronaldo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Togo alitumia nusu ya msimu wa 2010-11 akicheza kwa mkopo pale Santiago Bernabeu wakati Mourinho alipokuwa kocha wa klabu hiyo.

Na Adebayor amebainisha kwamba alishuhudia Mourinho akikwaruzana na Mreno mwenzake huyo.

“Tukiwa Real, tulikuwa tunaongoza kwa mabao 3-0 katika kipindi cha pili. (Mourinho) alikuja kwenye vyumba vya kubadilishia nguo na alionekana kama kichaa,” amebainisha Edebayor akinukuliwa na Gazeti la Daily Mail.

“Apiga friji, akaipiga televisheni, akamwaga maji. Alimuua kila mtu. Nakumbuka ‘alimuua’ Ronaldo baada ya kufunga mabao matatu[‘hat-trick’].

“Alisema, ‘Kila mmoja anasema nyinyi ni bora duniani na mnacheza vibaya. Nionyesheni ubora wenu. Ronaldo aliweza kufunga hat-trick lakini alizungumzia kuhusu yale aliyokosa.”






# STERLING AFUNGUKA TUZO YA MTAZAMO CHANYA YA UBAGUZI

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester City, Raheem Sterling, amesema ana matumaini kuwa mfano kwa wachezaji vijana baada ya kupata tuzo ya mtazamo chanya juu ya ubaguzi wa rangi.

Mshambuliaji huyo wa England ameyashutumu magazeti kwa namba yanavyowaandika wachezaji na kutaka adhabu kali kwa mashabiki wanaoonyesha ubaguzi wa rangi.

Alipewa tuzo hiyo Alhamisi usiku wakati wa kutangazwa kwa timu bora ya mwaka kwenye Ligi Kuu ya England.

“Wakati kizazi kipya kitakapokuja, unatakiwa kutengeneza mfano,” alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.

“Nikiwa nakuja hapa Liverpool nilizungukwa na watu kama Steven Gerrard ambao nilikuwa naowaona kama watu wa mfano. Kumuangalia yeye kunanifanya mimi nipiganie kuwa kama yeye.

“Unachukua vitu kadhaa kila mwaka, kujaribu na kuimarika dimbani.

“Nilikuwa nazungumza kuhusu uzoefu wangu binafsi, sikutarajia kuwa sehemu ya watu kunifuatilia.”

# Klopp: Liverpool ndio bora zaidi msimu huu

**LONDON,** England

KOCHA Jurgen Klopp amesema wachezaji saba zaidi wangeweza kuwapo kwenye kikosi cha mwaka cha wachezaji wa kulipwa, PFA, na amesisitiza “timu yangu ni timu bora ya msimu.”

‘Wekundu’ hao walishuhudia Andrew Robertson, Trent-Alexander Arnold, Virgil van Dijk na mshambuliaji, Sadio Mane wakichaguliwa kwenye kikosi cha mwaka cha wachezaji wa kulipwa, PFA kilichochaguliwa na wachezaji.

Manchester City walikuwa na wachezaji sita, huku Manchester United ikitoa mchezaji mmoja tu, Paul Pogba.

“Wangeweza kuwa wanne, watano, sita au saba zaidi,” alisema Klopp. “Walicheza vizuri zaidi kwa msimu mzima. Kwa upande wangu timu yangu ni bora kwa msimu.”

Wachambuzi wa soka wa BBC Sport, Gary Lineker, Alan Shearer na Jimmy Floyd Hasselbaink wote hawajakubaliana na uwezo wa Pogba kwenye kikosi hicho.

Nahodha wa Misri na mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah na nyota wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang ambao wote kila mmoja amefunga mabao 19 ya ligi msimu huu wameachwa kwenye kikosi hicho.

Pia nyota wa Tottenham, Harry Kane na mkali wa Chelsea, Eden Hazard ambaye wana mabao 17 na 16 kwenye Ligi nao hawamo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# POGBA, HAZARD KUTUA PAMOJA REAL MADRID

## PSG pia inaeleweka kuvutiwa na kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa...

**LONDON,** England

VIUNGO Paul Pogba na Eden Hazard wanatarajiwa kucheza pamoja katika kikosi cha Real Madrid msimu ujao kufuatia klabu hiyo ya Hispania kuamini itafanikiwa kupata saini ya nyota hao kutoka Manchester United na Chelsea majira haya ya joto, kwa mujibu wa chanzo cha Sky Sports.

Miamba hiyo ya Hispania inatarajiwa kukifanyia mabadiliko makubwa kikosi chake mwishoni mwa msimu, kufuatia msimu huu kuukosa ubingwa wa Ulaya na La Liga, na inaelezwa wachezaji hao wanaokipiga Ligi Kuu England, EPL ndio wanaoongoza katika orodha ya wanaosakwa na Real Madrid.

Pogba anakosolewa sana kwa kiwango chake kibovu hivi karibuni hapo Manchester United na anatarajiwa kuondoka kama watashindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**Hazard mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu na hajaonyesha ishara yoyote ya kuongeza mkataba, hiyo ikiwa na maana Chelsea itamruhusu kujiunga na Real endapo itafika dau lao la pauni milioni 100 inazohitaji ili kumwachia.**

Pogba alikaribia kujiunga na miamba hiyo ya La Liga wakati alipokuwa akiondoka Juventus miaka mitatu iliyopita, badala yake akajiunga na United pauni milioni 89.

Na wakati akiwa katika majukumu ya kimataifa mwezi uliopita, kiungo huyo mwenye umri wa miaka 26, alikiri kuichezea Real chini ya raia mwenza wa Ufaransa, Zinedine Zidane kutakuwa ni "ndoto kwa kila mtu".

Nahodha wa zamani wa United, Gary Neville aliiambia Sky Sports kwamba Pogba anataka kuondoka Old Trafford majira haya ya joto: "Sidhani kama anataka kuwa hapa, hilo ni tatizo. Wakala wake [Mino Raiola] yupo naye. Anaonyesha kipaji kwa Ole [Gunnar Solskjaer], na hadi sasa amefunga mabao 11 na kutoa pasi za mwisho saba ama zaidi."

PSG pia inaeleweka kuvutiwa na kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa.

Hazard, 28, pia amekuwa wazi kuhusu kiu yake ya kucheza Real wakati wa wasifu wake kisoka, akifafanua hilo kama "ndoto zangu tangu nikiwa mdogo".

Na kwa kuongeza, Mwandishi wa Ubelgiji, Kristof Terreur aliiambia Sky Sports kwamba Hazard anamuona Zidane kama anamhamasisha na kwamba kurejea kwa Mfaransa huyo kama kocha wa Real ina maana Hazard kutua Bernabeu "kumeangukia mahali pake".

## ZISIKUPITE

### YAJITOSA KWA RASHFORD

BARCELONA ipo tayari kuweka msukumo kwa kutoa pauni milioni 100 majira haya ya joto ili kufanikisha kumpata straika wa Manchester United na England, Marcus Rashford, 21. ***(Mail)***

### GOMES AWINDWA ARSENAL

ARSENAL inatarajia kutoa upinzani kwa wapinzani wao wa Ligi Kuu England, Everton katika mbio za kumsajili kiungo wa Barcelona, Mreno Andre Gomes, 25. ***(ESPN)***

### INTER KUMFUATA SANCHEZ

INTER MILAN itafunga safari kwenda kumsajili mshambuliaji wa Manchester United, Alexis Sanchez, 30, kama nyota huyo wa kimataifa wa Chile atakubali kupunguza mshahara wake. ***(Independent)***

### COUTINHO ATEGWA CHELSEA

CHELSEA itamgeukia kiungo wa Barcelona, Mbrazil Philippe Coutinho, kama itampoteza Eden Hazard majira haya ya joto. Hazard, 28, amekuwa akihusishwa na kujiunga na Real Madrid na 'Blues' inammulika Coutinho, 26, kama mbadala wake. ***(El Confidencial)***

### PSG YATAJA DAU LA MEUNIER

PSG inataka pauni milioni 26 kwa beki wa kulia Mbelgiji Thomas Meunier, 27, ambaye anawindwa na Manchester United, Arsenal na Chelsea. ***(Mirror)***

### SARRI AHOFU KUTIMULIWA

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri, anahofia kuwa anaweza kutimuliwa mwishoni mwa msimu. ***(Sun)***

### SOLSKJAER AMUONA DE GEA PSG

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anahofia kipa Mhispania David de Gea, 28, anataka kutimkia Paris St-Germain majira haya ya joto. ***(Sun)***

### RICHARLISON MAWINDONI UTD

MSHAMBULIAJI wa Everton na Brazil, Richarlison, 21, ni mchezaji wa mwisho kufikiriwa na Manchester United kama sehemu ya kukifanyia mabadiliko kikosi chake. ***(Telegraph)***

### AMSHUKIA SOLSKJAER

MAKAMU Mwenyekiti wa Manchester United, Ed Woodward, amemkosoa kocha Ole Gunnar Solskjaer na msaidizi wake, Mike Phelan wakati wa mazoezi kufuatia timu hiyo kukubali kipigo cha saba katika mechi tisa zilizopita waliposhuka dimbani kwenye mechi ya Manchester 'dabi'. ***(Mail)***

### ATLETICO YAMTAKA MATA

ATLETICO Madrid inapanga kumfuata kiungo wa Manchester United, Mhispania Juan Mata, 30. ***(Sport)***

### ARSENAL YAMGEUKIA BAILLY

ARSENAL inavutiwa kumsajili beki wa Manchester United na Ivory Coast, Eric Bailly, 25. ***(Mail)***

### EVERTON KUMSAJILI ABRAHAM

EVERTON ipo katika mbio za kumsajili straika wa Aston Villa, Muingereza Tammy Abraham, 21. ***(Star)***

HABARI MICHEZO

# KOCHA KMC AKIRI SIMBA KUWASHIKA

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Etienne Ndayiragije, amekiri kuwa timu yake ilizidiwa uwezo na kuwapa nafasi mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kupata ushindi wa mabao 2-1 katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini hapa.

Ndayiragije alitoa kauli hiyo muda mfupi baada ya kumalizika kwa mchezo huo na kuongeza kuwa Simba ilitumia vema nafasi walizopata katika mechi hiyo.

Kocha huyo raia wa Burundi alisema wachezaji wake walipambana kuhakikisha wanashinda mechi hiyo, lakini walishindwa kutimiza malengo yao ya kuondoka na pointi zote tatu.

**"Tulicheza kadri ya uwezo wetu, tulipambana na kucheza kwa bidii, lakini haikuwa bahati yetu, wao walianza kufunga na sisi tu kasawazisha, baadaye waka pata penalti na ndio wametu funga mechi hii," alisema Ndayiragije ambaye aliwahi kuifundisha Mbao FC.**

Naye nahodha wa KMC FC, Yusuf Ndikumana, alisema timu yao haikuwa na bahati katika mchezo huo licha ya kucheza vizuri na kwa umakini.

Ndikumana alisema bado wataendelea kupambana katika mechi zilizobakia za ligi hiyo kwa sababu wanahitaji kumaliza msimu huu wakiwa katika nafasi bora kwenye msimamo ambao unaongozwa na Yanga huku African Lyon ikiburuza mkia.

KMC FC inaendelea kuweka kambi yake jijini hapa kwa sababu inatumia Uwanja wa CCM Kirumba kama uwanja wake wa nyumbani baada ya Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kutumika katika michuano ya vijana wa umri chini ya miaka 17 (Afcon U-17) ambayo inamalizika Jumapili.




Beki wa KMC FC, Ismaili Gambo (chini), akijaribu kumdhibiti John Bocco wakati wa mechi ya Ligi Kuu Bara, iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba juzi na Simba kushinda 2-1. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# *Mbao waitangazia vita Ndanda FC*

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

IKIWA katika timu zilizoko kwenye janga la kushuka daraja, Kocha Msaidizi wa Mbao FC, Fulgence Novatus, amesema wamejipanga kuhakikisha wanashinda mechi yao dhidi ya Ndanda FC itakayochezwa Mei 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini hapa.

Mbao FC yenye pointi 37, iko katika nafasi ya 17 kwenye mzunguko wa ligi baada ya kucheza mechi 33 huku zinazofuata zikiwa ni Ruvu Shooting, Biashara United na African Lyon inayoburuza mkia.

Akizungumza na gazeti hili jana, Novatus alisema timu yake imekuwa ikifanya mazoezi kila siku bila kupumzika kwa lengo la kuwaimarisha wachezaji wake ili wapate matokeo mazuri katika mechi hiyo na nyingine zilizobakia.

Novatus alisema pia wamejipanga zaidi kuhakikisha wanashinda mechi zao tatu za nyumbani zilizobakia ikiwamo kuwakabili KMC FC kutoka jijini Dar es Salaam na Kagera Sugar ya Bukoba, Kagera.

"Tunahitaji ushindi wa aina yoyote katika mechi zetu zilizosalia ili kukaa katika nafasi salama, ushindani ni mkubwa lakini bila kupambana hatutaweza kutimiza malengo yetu, tunajua haitakuwa kazi rahisi kwa sababu hakuna anayejua nani atashuka mpaka muda huu," alisema Novatus.

Kocha huyo aliongeza kwa kuwakumbusha wachezaji wao kujituma ili kujitengenezea nafasi nzuri ya kubaki katika timu hiyo kuelekea msimu mpya wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kila mwaka.

Yanga yenye pointi 74, ndiyo iliyopo kileleni mwa ligi hiyo inayotarajiwa kumalizika Mei 28, mwaka huu kwa timu zote 20 kushuka dimbani siku hiyo ya funga pazia.

## Sita za Pemba zashuka daraja

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU sita za Ligi Kuu Zanzibar kutoka kisiwani Pemba tayari zimeshuka daraja msimu huu ambao unamalizika kesho, Jumapili.

Ligi Kuu ya Zanzibar msimu huu imeshirikisha timu 19 huku 10 zikitoka kisiwani Unguja na tisa zikitokea Pemba.

Timu hizo ambazo zinashuka daraja msimu huu ni Mwenge ambayo ipo nafasi ya 14 na alama 33, New star iliyopo nafasi ya 15 na alama 33, Opec nafasi ya 16 ikiwa na pointi 26, na Mbuyuni yenye pointi 22 ikiwa imejiweka katika nafasi ya 17.

Nyingine zilizoshuka ni Hardrock ipo nafasi ya 18 na alama 19 sambamba na timu ya Kizimbani ambayo ipo mkiani mwa ligi hiyo ikiwa na alama 11.

Aidha, timu zilizojinusuru kushuka daraja kutoka kisiwani Pemba ni Chipukizi ambayo ipo nafsi ya 11 ikiwa na alama 40, Selem View ambayo ipo nafasi ya 12 ikiwa na alama 38 na timu ya Jamhuri ambayo ipo nafasi ya 13 ikiwa na alama 37.

Kwa upande wa timu za Unguja ni Chuoni ambayo ina alama 46 ikiwa nafasi ya 10, Polisi ambayo ipo nafasi ya tisa na alama 46, Jang'ombe Boys iliyopo nafasi ya nane ikiwa na alama 53, Mlandege ambayo ipo nafasi ya saba ikiwa na pointi 70.

Timu nyingine ni Mafunzo ambayo ipo nafai ya sita na alama 70, huku nafasi ya tano ikichukuliwa na timu ya Malindi yenye alama 72, Maafande wa JKU ikishikilia nafasi ya nne na alama 73, nafasi ya tatu ikishilikiwa na Maafande wa Zimamoto wenye alama 73, nafasi ya pili ikienda kwa Maafande wa KVZ wenye alama 74 huku vinara wa ligi hiyo KMKM wakiwa na alama 77.

**MSIMAMO LIGI KUU BARA**



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 32 | 23 | 5 | 4 | 51 | 23 | 74 |
| 2.Simba | 26 | 21 | 3 | 2 | 55 | 11 | 66 |
| 3. Azam | 32 | 19 | 9 | 4 | 49 | 19 | 66 |
| 4. Mtibwa Sugar | 32 | 14 | 6 | 12 | 33 | 24 | 48 |
| 5. Lipuli | 33 | 12 | 12 | 9 | 30 | 28 | 48 |
| 6. Ndanda | 32 | 11 | 10 | 11 | 22 | 30 | 43 |
| 7. KMC | 33 | 9 | 15 | 9 | 33 | 25 | 42 |
| 8. TZ Prisons | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 9. Coastal Union | 33 | 9 | 14 | 10 | 29 | 33 | 41 |
| 10. Mbeya City | 32 | 11 | 7 | 14 | 31 | 34 | 40 |
| 11. Singida Utd | 33 | 10 | 10 | 13 | 24 | 32 | 40 |
| 12. Kagera Sugar | 33 | 9 | 12 | 12 | 28 | 35 | 39 |
| 13. JKT Tanzania | 32 | 9 | 12 | 11 | 20 | 27 | 39 |
| 14. Stand United | 33 | 11 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 15. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 16. Alliance | 33 | 9 | 10 | 14 | 24 | 36 | 37 |
| 17. Mbao | 33 | 9 | 10 | 14 | 19 | 33 | 37 |
| 18. Ruvu Shooting | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 19. Biashara United | 31 | 8 | 10 | 13 | 22 | 29 | 34 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |



Pogba, Hazard kutua pamoja Real

HABARI UK. 30



Baadhi ya wachezaji wa Simba wanaotarajiwa kuivaa Biashara United katika Uwanja wa Karume mjini Musoma leo, wakishangilia moja ya mabao yao katika Uwanja wa CCM Kirumba wiki hii. **PICHA: MAKTABA**

# Simba yampeleka Tuyisenge Yanga

●●● Kagere, Okwi, Bocco wachangia, sasa wafuata mkali wa kutupia nje ya boksi ambaye...

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

WAKATI ikiwa imeanza mazungumzo ya chini kwa chini na wachezaji wa hapa nchini kwa ajili ya kusajili ili kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu mpya, uongozi wa Simba umesema nafasi ya straika wa Gor Mahia, Jacques Tuyisenge imeota mbawa.

**Na kwa kauli hiyo ni wazi sasa Simba imeifungulia Yanga mlango wa kumsajili mshambuliaji huyo anayetisha kwa kutikisa nyavu Gor Mahia.**

Simba na Yanga, zote zilikuwa zikiwania saini ya Tuyisenge, lakini kikosi hicho cha mtaa wa Jangwani na Twiga kilijivuta nyuma kuhofia nguvu ya fedha ya Wekundu wa Msimbazi hao na sasa imeelezwa kimeanza mbio mpya za kumsajili. Awali kulikuwa na taarifa kuwa Simba, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara ilisaini mkataba wa awali na straika huyo raia wa Rwanda.

Akizungumza na gazeti hili jana, Afisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, alisema Kamati ya Usajili ya klabu hiyo imemuondoa Tuyisenge katika "rada" zake kutokana na uwezo wake kutofautiana sana na washambuliaji wao watatu tegemezi walioko sasa.

Magori alisema kuwa wameanza mipango ya kusajili mshambuliaji ambaye ana uwezo wa juu kuliko Bocco (John), Okwi (Emmanuel) au Meddie Kagere, ambao wameisaidia Simba kufika hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kiukweli Simba haina mpango na Tuyisenge, tunahitaji kuwa na mshambuliaji ambaye anawazidi kwa mbali Bocco, Okwi na Meddie, hawa wote ni wachezaji ambao wanacheza kwenye boksi, sasa anayetakiwa ni mwenye uwezo wa kufanya vitu vyote wakiwa nje ya boksi ili tufike tunakokuhitaji," alisema Magori.

Aliwataka wanachama na mashabiki wa Simba kutulia kwa sababu klabu yao imejipanga kuboresha kikosi hicho ili msimu ujao iwe na mafanikio zaidi katika mashindano ya ndani na kimataifa.

Hata hivyo, pia ndani ya klabu hiyo wapo wachezaji ambao wanamaliza mikataba yao na bado hawajui hatima yao kutokana na kutokamilika mazungumzo kuhusu kusaini mikataba mipya.

Mchezaji mmojawapo anayetajwa kurejea katika klabu hiyo ni nahodha na mshambuliaji tegemeo wa Yanga, Ibrahim Ajib.

# Aussems aiandalia Biashara dozi yake

**Na Somoe Ng'itu,** MUSOMA

IKIWA imevuna pointi sita jijini Mwanza, Simba kutoka Dar es Salaam inatarajia kuwakabili wenyeji Biashara United katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Karume mjini hapa.

Simba yenye pointi 66, inakutana na Biashara United katika mechi ya kwanza ikiwa ni kiporo na timu hiyo iliyopanda daraja msimu huu pamoja na Coastal Union na African Lyon.

Kocha Mkuu wa Simba Mbelgiji, Patrick Aussems, alisema jana licha ya wachezaji wake kuwa na uchovu, watacheza kwa umakini kuhakikisha wanapata ushindi na kuendelea kujisafishia njia ya kutetea ubingwa wa ligi hiyo wanaoushikilia.

Aussems alisema mabadiliko ambayo amekuwa akiyafanya katika timu yake yataendelea na yanasaidia kuwaweka vema nyota wake na kupata matokeo chanya kwenye kila mechi watakayocheza.

"Tumefika salama Musoma, na tunataka kupata ushindi katika mechi ya kesho [leo], tunajua Biashara United wako katika changamoto ya kushuka daraja, kwa hiyo tunatarajia kukutana na ushindani, ni wazi mchezo huu utakuwa mgumu," alisema mbelgiji huyo.

Amri Said, Kocha Mkuu wa Biashara United aliliambia gazeti hili kuwa wako katika nafasi mbaya na mchezo wa leo wanahitaji kushinda ili kufufua matumaini ya kubakia kwenye ligi hiyo inayoelekea ukingoni.

Said alisema wanafahamu na wamejiandaa kukutana na ushindani kutoka kwa Simba ambao wako katika harakati za kutetea ubingwa huku wakichuana na Azam FC pamoja na vinara, Yanga timu zote kutoka Dar es Salaam.

"Mechi ni ngumu kwetu na ni ngumu pia kwa Simba, ingawa kila timu ina malengo yake tofauti kuelekea za lala salama za msimu huu, wasitarajie mteremko, tumejiandaa kushinda mechi zetu zote zilizobaki za hapa nyumbani," alisema beki huyo wa zamani wa Simba.

Aliongeza kuwa wamepata muda mrefu wa maandalizi na kupumzika huku wakiisoma Simba tangu ilipokuwa inacheza mechi za kimataifa za Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo wawakilishi hao walitolewa katika hatua ya robo fainali.

Simba ambayo itaondoka mjini hapa leo usiku kwenda Mwanza kupanda ndege na hatimaye kesho asubuhi kurejea Dar es Salaam, itacheza mechi ya mzunguko wa pili dhidi ya Biashara United Mei 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >